MID WEEK JACKPOT!
TZS. 553,549,430
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Serikali** yafuta sherehe za miaka 59 ya Muungano

UKURASA 3




UKURASA 9

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 16, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581282
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**RIPOTI MAALUM**

# Tahadhari watumiaji vinywaji vya 'energy'

UKURASA 4

## Mvua zaleta adha usafiri, uharibifu wa miundombinu

UK. 2



Watembea kwa miguu wakipita kwa taabu katika maji yaliyotuama katika barabara ya Nyerere eneo la Karakana Vingunguti jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua kubwa kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 3

## MBARONI MADAI KUTENGENEZA NA KUSAMBAZA DAWA BANDIA



MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Mashariki, imemkamata mkazi wa Kipawa, Ilala jijini Dar es Salaam, Williams...




Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian    Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

## CAG abaini shida ukokotoaji tozo za magari ya nje TRA

UK. 2

MICHEZO NI SIKU YA HUKUMU UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# CAG abaini shida ukokotoaji wa tozo za magari ya nje TRA

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini makosa katika ukokotoaji wa tozo za magari ya kigeni katika Mfumo Fungamanishi wa Forodha (TANCIS).

Katika ripoti yake ya 2021/22 iliyowasilishwa Bungeni wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, amebaini hitilafu kadhaa kwenye kodi za magari ya kigeni yanayotoka nje ya nchi (transit vehicle) katika mfumo wa TANCIS, ili kuthibitisha usahihi wa kodi zilizokokotwa kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (1) na 7(2) cha Sheria ya kodi za magari ya kigeni yanatoka nje ya nchi, Sura ya 84 ya Sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

CAG anasema katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ya Mwaka 2021/22, CAG, hitilafu hizo ni magari 11,526, kati ya 143,792 (sawa na 8%) ya jumla ya magari ya kigeni yaliyotozwa kodi ni kiwango pungufu ya kilichotakiwa, kwa kiasi cha dola za Marekani 2,020,270.

Aidha, CAG anasema magari 7,501 kati ya 143,792 (sawa na 5% ya jumla ya magari ya kigeni) yaliyotozwa kodi, ambayo ni kiwango zaidi ya kilichotakiwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 698,528.

Pia anasema kulikuwa na majina yasiyo sahihi ya madereva, ambayo hayawezi kufuatiliwa iwapo yatakiuka kanuni na taratibu za usafiri zinazotumika.

Mfumo Fungamanishi wa Forodha, ni mfumo uliojengwa kwa misingi ya teknolojia ya hali ya juu, wenye lengo la kuongeza uthabiti, ufanisi, uwazi, na usahihi katika usimamizi wa forodha.

Kwa mujibu wa CAG, kwa kuwa ni mfumo wa unaotumia wavuti, TANCIS inawezesha shughuli za uendeshaji bila kutumia taarifa kwenye makaratasi. Hali hii inasababisha kupungua kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji na usimamizi wa forodha.

Kutokana na makosa hayo katika ukokotoaji wa tozo za magari ya kigeni katika mfumo wa TANCIS, CAG amependekeza kwa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), ihakikishe utimilifu wa taarifa na ukokotoaji wa kodi husika na kufanya mapitio ya usahihi wa tathmini ya kodi za magari ya kigeni yanayotoka nje ya nchi katika mfumo wa TANCIS,

Kwa kuweka mgawanyo wa majukumu katika utayarishaji, uthibitishaji na uidhinishaji, na ithibitishe umbali kati ya vituo vya mpaka katika mfumo wa TANCIS.



Waziri Mkuu na Mwenyekiti wa Kamati ya Sensa Kitaifa, Kassim Majaliwa akizungumza wakati wa uzinduzi wa machapisho ya Ripoti za Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)-Tunguu, jana. **PICHA:OFISI YA WAZIRI MKUU.**

# Mvua zaleta adha usafiri, uharibifu wa miundombinu

**Na Waandishi Wetu**

MVUA za masika zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali zimesababisha madhara yakiwamo nyumba 600 kuzingirwa na maji na barabara ya Segera-Tanga kukata mawasiliano.

Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema mvua kubwa zinazonyesha katika baadhi ya maeneo, zitaendelea mpaka Jumatano ijayo na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Katika mkoa wa Dar es Salaam jana, mvua hizo ziliathiri baadhi ya maeneo likiwamo eneo la Mtaa wa Faru, Kata ya Mnyamani wilayani Ilala na kusababisha zaidi ya nyumba 600 kuzingirwa na maji huku zaidi ya familia 1,500 zikiathirika.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Said Hassan, aliwaeleza waandishi wa habari jana kuwa mafuriko hayo yamesababishwa na njia za maji kuzibwa na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na hivyo, kukosa njia ya kupita na kwenda kwenye makazi ya watu.

"Mvua iliyonyesha kuanzia alfariji leo (jana) imeleta madhara makubwa kwa wakazi hawa. Maji yameingia ndani, vitu vimeloa na hawajui watalala wapi," alisema Hassan.

Mkazi wa eneo hilo, Mwanaisha Shomari, alisema amepoteza mali zake kutokana na maji kuingia ndani.

"Tunaomba serikali ichukue hatua za haraka kwa sababu tuna hatari ya kupata maradhi maana haya maji yamechanganyikana na ya vyoo," alisema Mwanaisha.

Katika hatua nyingine baadhi ya barabara mkoani humo jana, zilishindwa kupitika na kuleta usumbufu kwa watumiaji wake.

Katika barabara ya Umoja wa Mataifa, eneo la Selander, kuelekea Muhimbili, maji yalijaa na kushindwa kupitika kwa saa kadhaa.

Baadhi ya wananchi walilalamikia ubovu wa miundomboni ya maji taka katika baadhi ya maeneo ya jiji hilo, hali inayosababisha kuwapo kwa mafuriko.

Dereva wa gari katika eneo hilo, Lazaro Mollen, aliliambia gazeti hili kuwa, serikali inafumbia macho mifereji chakavu na mingine midogo na kusababisha kushindwa kumudu wingi wa maji.

"Hili tatizo siyo la leo wala jana, limekuwa tatizo sugu, mvua ikinyesha barabara inashindwa kupitika, inajulikana wazi sababu ni miondombinu chakavu isiomudu maji taka, lakini wanaotakiwa kufanyia kazi wapo kimya, mvua zikija tunalalamika zikikata tunakaa kimya," alisema Mollel.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Muliro Jumanne, kufahamu madhara ya mvua hizo kwa mkoa mzima lakini simu yake ya mkononi ikawa inaita bila kupokewa.

**BARABARA YAFUNGWA**

Video fupi iliyosambaa jana mtandaoni, ilionyesha mvua hizo zilivyoathiri miundombinu ya barabara ya Chalinze- Segera eneo kutoka Mbwewe kwenda Kimange na kusababisha mawasiliano ya barabara kukatika baada ya maji kupita juu.

Katika eneo hilo kulikuwa na kundi kubwa la watu wakiwamo wasafiri ambao baadhi walisimama upande wa pili wa barabara na wengine upande mwingine kutokana na maji yaliyosababishwa na mvua hizo kufunga barabara hiyo.

**TMA YATAHADHARISHA**

Katika taarifa ya TMA jana ilisema kwamba, mvua hizo zitaendelea kunyesha baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga, Pwani (vikiwamo visiwa vya Mafia) na Zanzibar.

Aidha, ilisema mvua hizo zinatarajiwa kuleta madhara kwa wananchi ikiwamo maeneo yao kuzungukwa na maji.

Mtaalamu wa hali ya hewa kutoka TMA, Joyce Makwata, alisema mvua hizo ni mwendelezo wa utabiri wa mvua zilizotolewa hivi karibuni.

"Tunawaomba wananchi kuendelea kuchukua tahadhari, mifumo ya hali ya hewa inaonyesha uwezekano wa kuwapo kwa mvua kubwa kwenye baadhi ya maeneo katika mikoa iliyotajwa kama tulivyotabiri kwenye utabiri wetu mwezi Februari mwaka huu.

"Vipindi hivi vya mvua kubwa vitaendelea kesho (leo) mpaka Jumatano, tunatarajia makazi ya watu yatazungukwa na maji, pamoja na uharibifu wa miundombinu lakini pia, baadhi ya shughuli za kiuchumi zitaathirika," alisema Makwata.

Alisema wananchi wanaokaa mabondeni pia, wanatakiwa kuchukua tahadhari kutoka na madhara yatakayotokana na mvua hizo.

Tayari mvua zilizonyesha usiku wa kuamkia jana kwenye baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam zimeleta athari kwa wananchi kwa maeneo mengi kuzungukwa na maji na kuathiri pia baadhi ya shughuli za kiuchumi.

TMA imesisitiza wananchi kuendelea kufuatilia taarifa wanazozitoa kupitia vyombo vya habari ili kuchukua tahadhari kwa maafa yoyote yanayoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Februari mwaka huu TMA, ilitoa utabiri wa mvua za Masika na kuonyesha upungufu wa mvua kwa baadhi ya mikoa lakini, ikatoa angalizo kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro kuwapo kwa vipindi vya mvua kubwa.

Katika utabiri huo mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma na mikoa yote ya Kanda ya Ziwa ulitarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani (mvua chache).

***Imeandaliwa na Mary Geofrey, Faustine Feliciane na Romana Mallya (Dar).**

HABARI KITAIFA

# Serikali yafuta sherehe Muungano kitaifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imetangaza kutokuwapo kwa maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa mwaka huu badala yake zitafanyika mwakani katika kuadhimisha miaka 60.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema jana kuwa hatua hiyo ni maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ametaka sherehe hizo zifanyike tofauti kwa kila mkoa kwa kufanya shughuli mbalimbali zikiwamo usafi wa mazingira na kupiga vita vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Majaliwa aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akitoa taarifa kwa wananchi kuhusu sherehe hizo katika hafla ya uzinduzi wa ripoti za sensa za mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsia.

"Kwa mwaka huu, hakutakuwa na sherehe za kitaifa bali kila mkoa utaadhimisha sherehe hizi hadi mwakani ambapo tutatimiza miaka 60 ya Muungano.

Hapo ndipo tutakuwa na sherehe za kitaifa tulizozoea," alisisitiza Majaliwa.

Aidha, alisema serikali inaelekeza shughuli za maadhimisho hayo kwa mwaka huu, zifanyike kwa siku 10 kuanzia kesho (Jumatatu).

Waziri Mkuu alitaja maelekezo mengine ni kwa majengo yote ya serikali kupambwa kwa vitambaa vyenye rangi ya bendera ya taifa, picha za waasisi wa Muungano na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Tanzania Bara.

Alisema hilo linatakiwa kufanyika pia upande wa Zanzibar kwa majengo kupambwa kwa rangi sahihi za bendera ya taifa na picha za waasisi wa Muungano na za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Majaliwa alisema katika maadhimisho hayo, mikoa na taasisi za serikali na vyombo vyote vya ulinzi na usalama, shughuli zao ziambatane na uzinduzi wa miradi ya maendeleo na masuala ya kijamii hususani upandaji wa miti, uchangiaji wa damu katika hospitali mbalimbali na vituo vya afya.

Pia alisema shughuli nyingine zitakazofanyika ni mashindano ya michezo ya sanaa mbalimbali, uandishi wa insha kwa shule za msingi na sekondari, kampeni ya kupiga vita unyanyasaji na ukatili wa kijinsia na ile ya kupambana na mmomonyoko wa maadili vikiwamo vitendo vya ushoga.

Waziri Mkuu alihimiza kuendelea kufanya mahojiano maalum na wazee maarufu wakiwamo wanawake, vyombo vya habari na vijana ili waujue muungano, sambamba na kufanya midahalo, makongamano kuhusu muungano na kuelezea hatua za maendeleo zilizofikiwa.

"Sherehe hizi zitafana vizuri zaidi, zile za kitaifa zitakapokuwa zimekamilisha miaka 60, eneo la kufanyia sherehe ya kitaifa litajulishwa baadaye," alisema.

Majaliwa alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili Wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, kulisimamia jambo hilo kwa kuhakikisha mambo hayo yanaratibiwa pande zote mbili kwa kuzishirikisha wizara, taasisi na idara zote.

Kaulimbiu ya mwaka huu katika sherehe za Muungano ni 'Umoja na Mshikamano Ndiyo Nguzo ya Kukuza Uchumi Wetu."



Mkaguzi wa Dawa kutoka TMDA, Japhari Mtoro (katikati), akiangalia dawa bandia na vifaa mbalimbali vilivyokutwa nyumbani kwa mtuhumiwa wa kutengeneza na kusambaza dawa mbalimbali za binadamu, William Mwangile, hayupo pichani nyumbani kwake Kipawa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MARRY GEOFREY**

# Mbaroni madai kutengeneza na kusambaza dawa bandia

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Mashariki, imemkamata mkazi wa Kipawa, Ilala jijini Dar es Salaam, Williams Mwangile (39), kwa madai ya kutengeneza na kusambaza dawa bandia za binadamu nyumbani kwake bila kibali.

Mkaguzi wa Dawa wa TMDA Kanda ya Mashariki, Japhari Mtoro, alisema hayo jana wakati wa operesheni hiyo iliyohusisha pia Jeshi la Polisi huku akibainisha kuwa mtuhumiwa huyo alikutwa na dawa mbalimbali, nembo na vifungashio vyake.

Alisema mtuhumiwa anadaiwa kutengeneza na kusambaza dawa hizo mijini, vijijini na nchi jirani na kwamba alikamatwa baada ya uchunguzi uliofanywa na TMDA.

"TMDA ilikuwa inamtafuta Williams Mwangile mkazi wa Matembele Lodge eneo la Kipawa kwa kosa la kuzalisha dawa bandia kwa mfumo wa makopo kinyume cha kifungu 76 cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura ya 219," alisema Mtoro.

Alisema baada ya kumkamata mtuhumiwa huyo, walimfanyia uchunguzi katika nyumba yake na nyumba ya wazazi wake.

"Nyumbani kwake tulikuta lebo (nembo) 537 ambazo zina majina ya dawa mbalimbali ambazo zimepigwa chapa lakini pia tulikuta makopo matupu 12 ambayo yanatumika kufungasha dawa," alisema Mtoro.

Alitaja vitu vingine kuwa ni viroba vitatu, kimoja cha unga wa njano na viwili unga mweupe.

Alisema nyumbani kwa wazazi wake, walikuta vifungashio vitupu ya dawa aina ya rangi mbili.

"Nyumbani kwa wazazi wake tumekuta lebo 142, hivyo kufikisha jumla ya lebo 679. Baada ya kumpata mtuhumiwa ataunganishwa na wenzake na kufikishwa mahakamani," alisema Mtoro.

Mkaguzi huyo aliwashukuru wadau na viongozi wa serikali ya mtaa, Jeshi la Polisi, wananchi kwa ushirikiano mkubwa walioutoa hadi kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ambaye walikuwa wakimtafuta tangu mwezi uliopita

Mjumbe wa Shina Na. 6 wa Mtaa wa Matembele ya Kwanza, Marygrory Mambo, ambaye ndiye aliyeshirikiana na TMDA na Jeshi la Polisi kwenye upekuzi huo, aliomba wananchi waendelee kutoa taarifa kwa mamlaka hiyo, kufichua wahalifu wa aina hiyo.

# Adaiwa kumuua mke kisa mali

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MKAZI wa Kasenga Muganda, Chato mkoani Geita, Dickson Jacob, anadaiwa kumuua mke wake, Kasaka January, kwa kumkata panga kwa kile kilichodaiwa kuwa ni mali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi (ACP) Safia Jongo, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana.

Alisema mtuhumiwa baada ya kutekeleza mauaji hayo, alitoroka na jitihada za kumtafuta zinaendelea.

"Chanzo cha mauaji ni kutokana na tamaa ya mali. Huyo mama alikuwa na mali na alikuwa na watoto ambao hakuzaa na mume wake kwa hiyo kitendo cha kuhudumia watoto wake hakikumfurahisha huyu mwanamume lakini pia huyu mwanamume amekuwa na tuhuma za kumwibia mali mke wake.

"Mtuhumiwa alikuwa anamilikiwa na huyo mwanamke na inaelezwa kuwa hivi karibuni alimwibia betri 40 za N 70 na baada ya kugundua alisema 'mwizi wangu nimeshamjua na nitamchukulia hatua', kauli hii ikachanganya na mengine. Tunaamini ndiyo chanzo cha mauaji haya," alisema Kamanda Jongo.

Alisema tukio hilo lilitendeka muda mfupi baada ya watoto wa marehemu kuondoka kwenye nyumba ya wazazi wao na walikuwa wanaangalia runinga na kwenda kwenye vyumba wanavyolala.

Baada ya muda mfupi, alisema walianza kusikia yowe ya mama yao akiomba msaada kutokana na mapanga aliyokuwa akikatwa.

"Baada ya kelele hizo, binti mmoja wa marehemu alisogea karibu kumsaidia mama yake lakini baba alivyofungua mlango alijaribu kumkata mtoto huyo na panga lakini alilikwepa ndipo baba huyo alipopata upenyo na kukimbilia kusikojulikana," alisema.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Deusdedith Katwale, amewataka wana ndoa kuheshimiana kwa misingi ya viapo vya ndoa zao badala ya kuendekeza migongano ya umiliki wa mali.

Mmoja wa ndugu wa karibu wa marehemu, Costantine Matogo, alidai kabla ya mauaji hayo, mtuhumiwa alijifungia ndani na mke wake kisha, kuanza kumshambulia kwa panga sehemu mbalimbali za mwili wake.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Chato, Madili Sakumi, amekiri kupokea mwili wa marehemu Kasaka.

Mauaji hayo yametokea ikiwa ni siku chache tangu wananchi wa Kata ya Muganza kuvunja na kukiteketeza kwa moto, Kituo cha Polisi maeneo hayo na kusababisha kukosekana kwa huduma za kipolisi.

Aidha, tukio hilo ni miongoni mwa matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi kinyume na sheria, licha ya serikali na wadau mbalimbali kuendelea kutafuta mwarobaini wa changamoto hiyo katika jamii.

# Tahadhari watumiaji kinywaji 'energy'

**Na Mary Geofrey**

WATUMAJI wa vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks), wako hatarini kupata madhara kiafya kutokana na kiasi kikubwa cha kemikali na sukari zinazotumika katika utengenezaji.

Mratibu wa Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Yohana Goshashy, ametoa angalizo hilo katika mazungumzo mahususi na Nipashe jijini Dar es Salaam.



Mratibu wa Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Yohana Goshashy.

Anasema vinywaji hivyo hutengenezwa kwa kuongeza kiasi kikubwa cha kemikali za kafeini, sukari na viambato vingine vikiwamo guarana, taurine, na L-carnitine, ndio maana watengenezaji wameandika tahadhari kwenye chupa.

Madhara yake, alisema ni kukosekana kwa usingizi, kupata kisukari, tatizo kubwa linalochangiwa na mtindo wa maisha.

Goshashy anasema utafiti wa vyakula lishe vikiwamo vinywaji hivyo, hakuna nchini ndio sababu matumizi yake ni holela. Anasema vinasababisha mtumiaji kupata kiu ya kutaka kuendelea kunywa mara kwa mara hivyo, kuendelea kuingiza sumu mwilini.


"Ukinunua vinywaji vya kuongeza nguvu, wametoa tahadhari kuwa usinywe zaidi ya moja kwa siku wakati wa kukaribia kwenda kulala kwa sababu zinakosesha usingizi. Watengenezaji wametimiza wajibu wao wa kutoa tahadhari, hivyo watumiaji ndio wanapaswa kuzingatia hayo," anasema Goshashy.

Anasema watu wazima kuanzia miaka 35 hadi 50 wanatakiwa kutumia miligramu 200 ya kafeini kwa siku. Kwa vijana, anasema wanapaswa kutumia miligramu 100 kwa siku na isizidi na ikitokea hivyo, husababisha madhara makubwa.

**MADHARA YA CAFFEINE**

Goshashy anasema mtumiaji akiwa ameathirika na matumizi ya vinywaji hivyo, anapata dalili za kichefuchefu, kutapika, kutetemeka, kukosa usingizi, kupata wenge, kichwa kuuma, kuharisha, kukosa usingizi, mapigo ya moyo kwenda haraka na kupoteza fahamu.

"Mtu wa aina hii ili awe sawa atatamani kuendelea kunywa vinywaji hii ili dalili hizi zote zikate na kuendelea kuwa kawaida," anasema Gashoshy.



Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, madhara pia ya kuacha kutumia mtu hupata madhila ambayo yamfanya kujisikia kichefuchefu, kutapika, kukosa usingizi na mapigo ya moyo kutokwenda sawa.

"Hizi dalili utaziona ukiacha kutumia vinywaji hivi kwa saa 12 hadi 24 na ili mtu awe sawa anatamani kunywa na akinywa anajisikia vizuri tena," anasema.

Anabainisha zaidi kuwa kuwa vinywaji vya kuongeza nguvu pia, vinasababisha mtu kujihisi hayuko sawa kama kuna kitu alichopungukiwa mwilini, hivyo kumlazimu kuendelea kunywa.

Anasema chai pia ina kafeini ambayo haizidi miligramu 50 ndiyo maana haizuiwi kuendelea kutumiwa kwa kuwa kiwango chake ni kidogo kulinganisha na vinywaji vya kuongeza nguvu.

Mtaalamu huyo anasema kuna vinywaji vya kuongeza nguvu ambayo vina zaidi ya caffeine' 80 ambayo ikitokea mtu anakunywa mbili kwa siku, anakuwa ametumia miligramu 160 nje ya kiwango cha matumizi kinachoshauriwa na wataalam wa afya isizidi miligramu 100 kwa vijana kwa siku.

**MATATIZO MAKUBWA**

Vinywaji hivyo, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, vinaweza kusababisha matatizo kwa mtumiaji kama vile kupata magonjwa ya moyo, shinikizo la juu la damu hali inayosababishwa na mishipa inayopitisha damu kwenda kwenye moyo kushindwa kufanya kazi vizuri.

Pia anasema mtumiaji anaweza kupata ugonjwa wa kupoooza, kupunguza uzito wa chembe sahani za damu na matatizo makubwa kusababisha kupasua mishipa ya kusafirisha hewa ya oksijeni.

Matatizo mengine, anayataja kuwa ni mtu kupata wasiwasi mkubwa, kukosa hamu ya kula kwa muda mrefu inayomlazimu kuendelea kunywa kinywaji hivyo ili mwili kupata nguvu.

Goshashy anasema 'caffeine' iliyomo kwenye vinywaji hivyo, husababisha mtumiaji kupata haja ndogo mara kwa mara na kupunguza maji mwilini na wakati mwingine kuathiri figo.

"Mwili unapoteza maji hivyo, figo kufanya kazi kubwa ya kuchuja taka na mwisho wake kuchoka na kushindwa kufanya kazi yake vizuri. Hii ni kwa wale ambao wanatumia kofeini zaidi ya miligramu 300 kwa siku ambayo ni zaidi ya vinywaji hivyo vitatu kwa siku," anasema Goshashy.

Pia anabainisha kwamba sukari iliyomo kwenye vinywaji hivyo ni nyingi na yenye glukozi nyingi zaidi ambayo husababisha kuwapo kwa sukari nyingi kwenye msukumo wa damu.

"Wengi wanakunywa wakiwa wametoka kwenye kazi ngumu na mwili ukiwa umechoka. Sukari hutakiwa kuingia mwilini taratibu, sasa unapokunywa vinywaji hivi, unapeleka sukari nyingi kwa haraka, hivyo kuzalisha tatizo," anabainisha.

Anataja athari nyingine mwilini ni kupunguza madini ya sodium ambayo kazi yake ni kusafirisha damu, kuchuja na hivyo kuharibu mfumo wa mwili, kushindwa kufanya kazi sawasawa.

**FAIDA**

Pamoja na madhara hayo, Goshashy anasema vinywaji hivyo pia fina faida mwilini ikiwamo kuufanya mwili kuwa mchangamfu wakati wote na kuweka kumbukumbu sawa. Pia anasema husaidia kuongeza umakini na uwezo wa kufanya kazi kwa kuwa anakuwa na ari ya kutosha.

**ATOA USHAURI**

Mtaalam huyo anashauri watu, hasa vijana, kuendelea kula vyakula vinavyoongeza nguvu mwilini ili kuwaondolea utegemezi.

Anaonya kwamba vinywaji hivyo, haviongezi nguvu za kufanya tendo la ndoa isipokuwa vinaupa mwili nguvu wa kuwa na uwezo wa kushiriki tendo hilo.


Anasema jukumu la GCLA ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuacha matumizi hayo ambayo madhara yake ni makubwa kwa vijana na Taifa kwa ujumla.

**WATUMIAJI WANENA**

Jumanne Ismail, ambaye ni mmoja wa watumiaji wa vinywaji hivyo, anasema fani yake ni teknolojia ya habari (IT), hivyo humfanya akae muda mrefu kwenye kompyuta na kwamba kinywaji hicho humwondolea uchovu.

Mjasiriamali Mahmud Jumbe anasema amekuwa akitumia kinywaji hivyo ili kupunguza usingizi.

Dereva wa roli, Moses Ismail, anasema: "Kwenye kazi yangu ninahitaji kinywaji chupa mbili na bazooka ambazo ninakunywa nikiwa naendesha gari kutoka kutoka Dar es Salaam hadi Kahama. Nisipotumia kinywaji hiki ninasinzia," anasema.



## HABARI KITAIFA

# Mtoto auawa madai kujihusisha wizi, ubakaji

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MTOTO Michael Chapa (15) mkazi wa mtaa wa Kivukoni, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, ameuawa na wananchi kwa madai ya kuwa mmoja wa vijana waliomo katika kikundi kinachojihusisha na wizi na ubakaji, maarufu kama 'Damu Chafu'.

Tukio hilo limetokea baada ya wizi, uporaji wa simu, fedha, ubakaji na watu kujeruhiwa kukithiri katika Kata ya Shanwe, Mtaa wa Kivukoni mjini hapa.

Mtoto huyo ameuawa zikiwa ni siku chache baada ya mtu mmoja kuvamiwa na kukatwa sikio na kikundi hicho ndipo wananchi walipowatafuta wahusika.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema jana kuwa kabla ya Chapa kupigwa, walipigwa vijana wengine wawili na kutakiwa kutaja wanaofanya nao uhalifu huo.

Walisema ndipo siku iliyofuata alikamatwa Chapa na kushambuliwa na wananchi waliokuwa na silaha za jadi hadi kusababisha kifo chake.

"Jana (juzi) walipitishwa vijana wawili hapa mmoja mdogo mwenye umri kama miaka tisa, alikuwa anatema damu baada ya kipigo, wakawaacha. Leo (jana) ninatoka kwenye kazi zangu, nikakuta watu wamejaa kuuliza wakasema 'Damu Chafu' anapigwa.

Niliposogea nikamwona Chapa yuko hoi na ilipofika saa 4:00 usiku akafariki dunia," alisimulia Clement Pius.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Titus Chapa, alisema alipigiwa simu akiwa shambani akajulishwa kuwa mtoto wake amepigwa na ilipofika majira hayo akapata ujumbe mwingine kwamba amefariki dunia.

"Kabla ya tukio hili, siku moja polisi walikuja usiku wa saa 7:00 na kuniuliza wapi aliko? Wakati huo sikujua aliko kwa kuwa hakuwamo ndani. Nilikamatwa na kupigwa sana nikiwa na vijana wengine hao wanaodaiwa kuwa ni 'Damu Chafu' kisha nilitoa Sh. 50,000 na kuachia," alisema baba huyo.

Alisema wamekuwa wakimsihi mtoto wake na ndugu wengine kuwa aachane na kazi hizo na aliwahi kumtaka waende wote shambani lakini aligoma.

"Mimi na wadogo zake na mama yao tukahamia shambani, yeye tukamwacha hapa. Yaliyoendelea huku sijui hadi leo (jana) kuambiwa ameuawa,"alisimulia mzazi huyo.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kivukoni, Kabambi Zacharia, alikiri kutokea kwa mauaji hayo na kwamba vitendo vya uhalifu vimekithiri mtaani hapo na wazazi wamekuwa hawana ushirikiano na viongozi ili kuwafichua.

Wakazi wa mtaa huo wameiomba serikali kuingilia kati ili kutatua tatizo hilo huku wakisema hawana amani na nyumba zao wala hawawezi kutembea nyakati za usiku kwa kuhofia kupigwa na vijana hao na kuporwa mali zikiwamo fedha pamoja na kufanyiwa vitendo vya ubakaji hasa wanawake.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, lilisema misako na doria iliyofanyika ilikamata vijana 15 na kufikishwa mahakamani na baadhi wakitakiwa kulipa faini ya Sh. 50,000.

# Waathirika tope la mgodi walipwa fidia

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI walioathirika na tope la bwawa la mgodi wa almasi wa Williamson Diamond Ltd (WDL) wilayani Kishapu wamelipwa fidia zao.

Meneja Uhusiano wa mgodi huo, Bernard Mihayo, aliyasema hayo jana wakati mchakato wa ulipaji fidia kwa wananchi walipoteza vitu vyao kwa kufunikiwa na tope ukiendelea.

Alisema mpaka sasa mgodi umeshalipa fidia kwa asilimia 97 na kati ya watu 304, tayari 294 wameshalipwa na waliosalia ni wale ambao bado wana migogoro ya kifamilia ambayo wakiimaliza watalipwa.

"Mpaka sasa tumeshalipa fidia kiasi cha fedha Sh. bilioni 1.8 kwenye akaunti zao na leo (jana) tunalipa vitu vya waathirika ambavyo vilipotea kwa kufunikwa na tope, na mwezi Juni tutajenga nyumba 47," alisema Mihayo.

Alisema fidia zilizotolewa ni pamoja na vitanda, majembe, jenereta kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, baiskeli, pikipiki, mabati, magodoro na chakula.

Kwa mujibu wa Mihayo, Juni hadi Julai, mwaka huu, wataanza kulipa fidia za mazao, kwa kutoa chakula kutokana na waathirika hao ambao hawakulima baada ya mashamba yao kufunikwa na tope na watapewa kwa awamu mbili.

Baadhi ya waathirika hao akiwamo, Jomu Makunze, ambaye amefidiwa pikipiki, alisema hakuamini kama watalipwa na kuushukuru uongozi wa mgodi pamoja na serikali.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashaurui ya Wilaya ya Kishapu, Grace Mwandu, alitoa wito kwa wananchi na kusema fedha ambazo wamezipata wazitumie kwa madhumuni kusudiwa.

Novemba, mwaka jana, bwawa hili la kuhifadhia maji machafu, lilipasuka kingo zake na kutiririsha tope ambalo lilivamia mkazi ya watu na kuathiri zaidi ya vijiji vya Ngw'anholo na Nyenze, lakini hakuna mtu aliyepoteza maisha.


**FANIKIWA MICROFINANCE LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA**

**Work ethic company limited, Tulvin na Tanfin** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Gari jijini la Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Theofrida Joseph Masau | TOYOTA HARRIER-T512DMJ | 29.04.2023 |
| Benezeth Kyaruzi Benedict | MAZDA BONGO-T221 | 29.04.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315 (Work ethic) au 0677014355 (Fanikiwa)**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha BUNJU Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 575/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CHAUSIKU JUMA MWINYIMVUA WA BUNJU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DIWANI MAGUNO MWINYIMVUA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 nwezi 04 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia, endapo kuna mtu yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa *Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa * Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika imetolewa leo tarehe 12 mwezi 04 mwaka 2023



IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR MARA
AT MUSOMA

MISC. APPLICATION NO. 322 OF 2021

TUJIENGE TANZANIA .................................. APPLICANT

VERSUS

1. KICHERE NGOCHOGE
2. TWALIB ALLY ........................ RESPONDENTS

**SUMMONS/NOTICE**

**TO,**
**1. KICHERE NGOCHOGE**
**2. TWALIB ALLY (RESPONDENTS)**

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the Application which is obtainable from the registry of this Tribunal. **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person (s) or by recognized agent(s) for mention on 27th April, 2023 at 08:00am in the forenoon.

**TAKE NOTICE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.

Given under my hand and seal of this Tribunal this .................. day of .................., 2023.

Kitungulu, E.
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara



**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**MATRIMONIAL APPEAL/CAUSE NO 61 OF 2023**

**VICTORIA FRUMENCE SAMKY PETITIONER**

**VERSUS**

**SERAPHINE AUGUSTINO RIMSI RESPOMDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 16 day of 05 2023 at 8:30 am Before MSAFIRI SRM

Your required to appear in this Court without Failure and you must produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support of your Case.

GIVEN under my hand and Seal of the Court this 13 day of 04 2023.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

COPY TO BE SERVED UPON



# KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**FLEX FRANK MSHIU** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya **TVS** zenye usajili namba **MC 924 CQM** na **MC617CTY**. kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**KAWE POLICE**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MADAI NA ..11/2023**

**SHINDA JULIUS MAYENGA..............................MDAI**

**DHIDI YA**

**LEONARD A MKONY.................MDAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**LEONARD A. MKONY**
**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 21/04/2023 saa2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.
Endapo hutofika wewe binafsi ama Mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 13 mwezi 04 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MOROGORO.



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI**
**WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUSUDIO LA KUTOHUISHA MILIKI YA ARDHI**

**WAMILIKI ALIOANDIKISHWA: MUSA DAMIAN MWINSHEHE wa S.L.P 267 MOROGORO na ndugu SAD ISMAIL MAGWAILA wa S.L.P 126 MOROGORO**
ARDHI: **KIWANJA NA. 162 BLOCK 'A' KIGURUNYEMBE MOROGORO MUNICIPALITY**
**MUOMBAJI:** ISDORY SILVERY LUANDA wa S.L.P 398 MOROGORO ambaye ameuziwa na ndugu DONALD LUSATO KURWIJILA wa S.L.P 3064 MOROGORO
Taarifa inatolewa kwamba ARDHI iliyotajwa hapo juu tunakusudia kutokuhuisha miliki yake kwa waliokuwa wamiliki wa awali ndugu MUSA DAMIAN MWINSHEHE wa S.L.P 267 MOROGORO na ndugu SAD ISMAIL MAGWAILA wa S.L.P 126 MOROGORO
Zaidi sana ofisi inakusudia kumilikisha ndugu ISDORY SILVERY LUANDA wa S.L.P 398 MOROGORO ambaye ameuziwa na ndugu DONALD LUSATO KURWIJILA wa S.L.P 3064 MOROGORO
Iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
MAELEZO yeyote, yaelekezwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA - MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.

AMBARA HP
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO



# KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SELEMANI ABDALLAH NZIMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T697 ADW.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

POLISI TAARIFA:
**DAR/MBA/RB/132095/2023**



# KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA SWALEHE BAKARI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S3691/0119/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ANNA MKAPA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015.kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIM/RB/130766/2023**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari zichukuliwe ili kuepusha madhara ya mvua

**MVUA** za masika zinaendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini huku zikiripotiwa athari mbalimbali zikiwamo nyumba kuzingirwa na maji, kuanguka na watu kupoteza maisha. Sambamba na hayo, kuna baadhi ya maeneo hususan Dar es Salaam barabara zikiwa zimejaa maji, hivyo kusababisha wapita njia kupata adha ya kuvuka barabara na hata magari kushindwa kutembea vizuri.

Jana, mathalan, mkoani Dar es Salaam katika maeneo kadhaa yakiwamo Buguruni Mnyamani, mvua iliyonyesha kuanzia alfajiri ilisababisha zaidi ya nyumba 600 kuzingirwa na maji. Aidha, katika barabara ya Nyerere eneo la Vingunguti, maji yalijaa barabarani kiasi cha kufanya magari kupita kwa shida pamoja na waenda kwa miguu.

Katika barabara kuu ya Chalinze- Segera kati ya Mbwewe na Kimange, mvua hizo zilisababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara, hivyo kusababisha safari za magari kusimama kwa saa kadhaa.

Hayo ni madhara ambayo yamepatikana kwa siku moja tu na kwamba kuna uwezekano wa athari zaidi kutokana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutabiri kuwa mvua kubwa kama zilizonyesha jana maeneo mbalimbali hususani ukanda wa pwani, zinaweza kunyesha mfululizo hadi Jumatano ijayo.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka hiyo imetoa rai kwa wananchi kuchukua tahadhari kutokana na majanga yanayoweza kujitokeza. Licha ya kutoa tahadhari hiyo, TMA pia imewataka wananchi kufuatilia taarifa zinazotolewa na taasisi hiyo kupitia vyombo vya habari ili kujihami dhidi ya maafa yoyote yanayoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ziko sababu mbalimbali ambazo zimefanya maeneo mbalimbali kukumbwa na athari za mvua kila zinaponyesha zikiwamo ujenzi holela wa makazi, miundombinu chakavu ya maji machafu hususan mifereji inayosafirisha maji machafu yakiwamo ya mvua pamoja na shughuli za kibinadamu. Sambamba na sababu hizo, ujenzi wa barabara ambao haukuzingatia athari za kimazingira pindi mvua inaponyesha na utupaji ovyo wa takataka pia vinachangia.

Katika mkoa wa Dar es Salaam, kwa mfano, sababu zilizotolewa kuhusu nyumba kuzingirwa eneo la Buguruni Mnyamani ni ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unaoendelea ambao umefanya maji kuacha njia yake na kuingia kwenye makazi ya watu.

Kutokana na TMA kutoa tahadhari kuwa mvua zinatarajiwa kunyesha kwa siku kadhaa, kuna umuhimu wa kuchukua hatua katika maeneo mbalimbali hasa yale ambayo yamekuwa yakisababisha maafa kila zinaponyesha hasa wakati wa masika.

Ni dhahiri kwamba suala hili ni mtambuka kwa maana linawahusu watu wote pamoja na serikali, hivyo kila mwanajamii anapaswa kuchukua tahadhari ikiwamo kuhakikisha mifereji inayopitisha maji ya mvua inakuwa safi wakati wote. Suala hili ni muhimu zaidi kwa mkoa wa Dar es Salaam ambao katika maeneo mengi mifereji hiyo haifanyi kazi.

Kwa maeneo ambayo barabara kuu zinapita kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine, Wakala wa Barabara (TANROADS) inatakiwa kufanya uchunguzi wa maeneo ambayo ni korofi wakati wa mvua na kuchukua hatua ikiwamo kutengeneza makalavati ili kuruhusu maji kupita bila kuathiri usafiri wa mabasi na magari mengine.

Hatua hizo ni za muda mfupi lakini kuna mambo ya kufanya kwa ajili ya nyakati zijazo kama vile ujenzi unaozingatia athari za mazingira, kutumia wataalamu katika fani mbalimbali na kuweka miundombinu katika hali ya usafi na usalama ambayo ni rafiki wa mazingira.

Ni wazi kwamba iwapo kila mmoja, kwa maana ya taasisi za serikali na binafsi, mamlaka za serikali za mitaa na wananchi kwa ujumla watachukua hatua, maafa yatokanayo na mvua yatakuwa historia labda ziwe zile kubwa kama El-Nino ambazo zilitikisa nchi miaka ya 1990 .

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Majanga ya asili hayaepukiki, lakini tahadhari ni muhimu

**MAFURIKO** ya mvua ni miongoni mwa majanga ya asili, ambayo yamekuwa yakiikumba baadhi ya mikoa na kusababisha madhara ikiwamo watu kupoteza mali zao au wakati mwingine baadhi yao kufariki dunia.

Hivi karibuni mafuriko hayo yamevikumba baadhi ya vijiji katika mikoa ya Mtwara, Rukwa, Mara na maeneo mengine na kusababisha vifo vya watu, mifugo, uharibifu wa vyakula na kuharibu makazi.

Kwa mfano, zaidi ya watu 1,800 wameathiriwa na mafuriko mkoani Mtwara baada ya mvua kubwa kunyesha katika wilaya za Mtwara na Newala, na kwamba zaidi ya 1,400 wameokolewa katika wilaya ya Mtwara katika Kijiji cha Kivava, huku wilayani Newala wakiokolewa watu 300.

Inaelezwa kuwa wananchi wengi wanaishi mashambani ambapo baadhi ya maeneo yalifunikwa na maji ya mvua hivyo wakalazimika kukusanyika katika eneo la mlima ili kujihifadhi, huku baadhi ya nyumba zikiwa zimebomoka.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Newala, Alhaji Rajab Kundya, kaya 528 katika vijiji na vitongoji vya Kivukoni na Sokoni, wote wamehamishiwa shule ya Msingi Kivava, kwa ajili ya kuangalia usalama wao na mali zao.

Wakati hayo yakijiri huko, wiki hii watu saba walifariki dunia, wengine 21 kukosa makazi kutokana na mto Talanda katika Kijiji cha Talanda Kata ya Milepa wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa kujaa na kufurika.

Taarifa zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Talanda, Oscar Denya, kwa vyombo vya habari ni kwamba waliofariki ni wanaume watatu na wanawake wanne wa familia mbili tofauti.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sixtus Mapunda, anasema serikali imewahamisha wananchi wa kaya 10 ambao nyumba zao zote zimesombwa na maji na kuanza kuwajengea nyumba sehemu nyingine.

Katika hali hiyo, ni wazi kwamba ingawa majanga ni suala la kuchukua tahadhari ikiwamo kutojenga nyumba katika maeneo hatarishi ni la muhimu ili salama badala ya kung'ang'ania kwenye hatari.

Utabiri wa hali ya hewa ni mojawapo wa nyenzo muhimu zinazoweza kuokoa maisha na pia kuepusha madhara makubwa yatokanayo na uharibifu wa miundombinu baada ya mvua na mafuriko.

Kimsingi, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imekuwa ikijitahidi kutoa tahadhari kwa watu wanaoishi maeneo ambayo si salama, lakini baadhi ya watu hushindwa kuzingatia utabiri huo na kujikuta wakikumbwa na mafuriko.

Ninatambua kuwa majanga mengine hayaepukiki, lakini watu kuchukua tahadhari ni jambo kwa kufuata maelekezo ya wataalam wa hali ya hewa ni jambo muhimu linaloweza kuwafanya watu kuwa salama.

Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) hasa lengo namba 13, serikali na mashirika mbalimbali yanahimizwa kuchukua hatua za haraka zinazoweza kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Bahati nzuri hatua zimekuwa zikichukuliwa kwa kuwekeza katika sekta ya utabiri wa hali ya hewa, kwa kununua vifaa vya kisasa na pia kutoa elimu katika baadhi ya vyuo vikuu kuhusu utabiri huo.

Lengo kubwa likiwa ni kutaka Watanzania waelewe athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchukua hatua za kuziepuka kadri inavyowezekana, ingawa kama nilivyoeleza awali, majanga mengine ya asili hayaepukiki.

Kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam, wanajua jinsi ambavyo jiji limekuwa likizidiwa na wingi wa maji hadi katika majumba yao na kusababisha mafuriko pale mvua inaponyesha.

Miongoni mwa sababu zinazochangia mafuriko hayo, ni baadhi ya watu kujenga nyumba kwenye mikondo ya maji ya mvua, ubovu wa miundombinu ikiwamo kuziba kwa mitaro ya kupitisha hayo.

Pamoja na mambo mengine, ninadhani jambo la msingi katika yote ni kila mmoja kuchukua tahadhari kadri inavyowezekana ili kuokoa maisha, kwa kuwa majanga hayana hodi na ni hatari kwa binadamu na viumbe vingine.

Kwa njia hiyo, hata kama mvua itakuwa kubwa, athari zake zinaweza kuwa kidogo kuliko ilivyo sasa ambapo ikinyesha inabomoa nyumba, watu wanakosa makazi na kuharibu mashamba.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Kwa nini tunakubali madudu ripoti ya CAG kila mwaka?



**Pascal Mayalla**

KATIKA makala hii, naendelea na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) nikijikita jinsi sisi Watanzania wakiwamo Wabunge wetu, walivyohamanika nayo kwa kushadadia taarifa za ufisadi.

Katika kufanya hivyo, wanataka kuuhabarisha umma kwamba sasa ufisadi ndio umeongezeka sana, wakati kiuhalisia kwa takriban miaka 10 mfululizo, ripoti za CAG zinaonyesha ufisadi na tena zingine ufisadi mkubwa na wa kutisha kuliko huu ambao umesababisha nijiulize je, kuna uwezekano baadhi ya sisi Watanzania ni wajinga?

Mtu mwenye akili timamu na busara, anapojikwaa mahali na kuanguka, akiamka si tu anaangalia alipoangukia, bali mahali alipojikwaa ili kupata sababu iliyomfanya ajikwae na kuanguka. Baada ya hapo, anaamka na kuendelea na safari yake.

Huko mbele anaweza kuja kujikwaa tena pale pale alipojikwaa mwanzo na kuanguka tena na safari hii si akajikwaa tu na kuanguka na hatimaye kuinuka na kuendelea na safari yake, bali anaweza akaanguka na kuumia hata akashindwa kuinuka na kuendelea na safari yake. Safari yake inakuwa imeishia hapo.

Hiki ndicho Watanzania wanachokifanya kwenye ripoti ya CAG. Ni ripoti ya matokeo tu ya ukaguzi baada ya kuibiwa na si chanzo.

Siku zote tunasisitiza ili Tanzania tupate maendeleo endelevu ya kweli, tunahitaji mifumo imara yenye uwazi na uwajibikaji ikiwamo mfumo wa kudhibiti kabla hatujaibiwa badala ya kuipa fedham ijizi na kuiangalia inavyotafuna, kisha mnakuja kukagua na kutoa ripoti ya CAG kuonyesha tumeibiwa.

Hapo tunapaswa kujiuliza nini wajibu wa CAG kama mdhibiti? Mbona bado tunaibiwa tu na Tanzania kuendelea kufanywa shamba la bibi? Je, sisi Watanzania baadhi yetu ni wajinga, yaani vichwa vitupu kabisa na wengine ni vichwa maji? Nasema hivi kwa sababu, kwa muktadha wa ripoti ya CAG, inaonekana idadi yetu kubwa uwezo wa kufikiri (logical thinking) na kufanya tafakuri tunduizi (critical analysis) ni mdogo.

Ni dhahiri kwaba wengi wetu hatuna uwezo wa kufanya uamuzi sahihi kwa wakati sahihi, hali inayosababisha ripoti za CAG kila mwaka kuwa na madudu yale yale mwaka hadi mwaka. Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana hata ripoti ya mwaka huu watu ndiyo wanajifanya wakali, wanashangaa! Wanashangaa nini wakati ripoti zote za CAG zina ufisadi?

Kila ripoti ya CAG inaandamana na mapendekezo ya CAG na Bunge letu linajadili na kutoa Azimio la Bunge na kupeleka serikalini kwa utekelezaji lakini hakuna mrejesho wa nini kimetekekezwa mpaka ripoti ya CAG ya mwaka unaofuata ina madudu yale yale yakijirudia. Kwa mantiki hii, hili linaashiria nini?

Kumuita mtu yoyote kuwa ni mjinga au mpumbavu, kama huyo mtu hayuko hivyo ni kumtukana na si jambo zuri lakini kama mtu huyo kweli ni mjinga au ni mpumbavu, si kumtukana bali ni kumwambia ukweli. Mwalimu Julius Nyerere, mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, alitumia neno "wajinga".

Rais wa awamu ya tatu, mzee Benjamin Mkapa, alitumia neno 'Wapumbavu' na Rais Samia Suluhu Hassan ametumia neno 'stupid'.

Naomba kuweka wazi kuwa kwenye andiko hili, sijamtukana mtu yeyote wala sijawaita watu ni humu kuwa ni wajinga au wapumbavu bali nimeuliza tu swali kuwa kuna uwezekano sisi Watanzania ni wajinga au waopumbavu?

Majibu ya swali hili ndiyo yatakayosema kama kweli sisi tuko hivyo au la. Haiwezekani kabisa kwa watu wenye akili timamu, wakafanyiwa mambo ya ovyo na ya ajabu kama yaliyomo kwenye ripoti ya CAG ya mwaka hadi mwaka kwa kufanyiwa madudu yale yale halafu mwaka unaofuatia yakajirudia na wasifanye kitu.

CAG ni mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za fedha za serikali, hivyo kazi yake ni kwanza kudhibiti na baadaye kukagua. Mbona tunaletewa ripoti tu ya ukaguzi baada ya matumizi mabaya ya fedha za serikali lakini hakuna ripoti yoyote ya CAG kwamba alidhibiti nini?

Kwa mujibu wa Ibara 153 (3) fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hazitatolewa kwa ajili ya matumizi mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na CAG na pia kwa sharti kwamba ziwe zimetolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Je, umefika wakati sisi Watanzania badala ya kushadadia Ripoti ya CAG ya ukaguzi wa hesabu za serikali, tuombe kupewa na ripoti ya udhibiti tuone CAG wetu alidhibiti nini?

Watanzania tupatiwe ripoti ya thamani ya fedha (value for money) si tu kwa kila fedha za miradi bali hata fedha za matumizi ya kawaida. Kuna zabuni za vitu vya kawaida kwa matumizi vya kawaida vya ofisi ambazo zina bei za ajabu. Ofisi ya CAG itoe elimu kwa umma kuwa si kila ongezeko la gharama ni wizi na upigaji, kwa kuwa ogezeko lingine la bei ni halisi.

Si kila ripoti chafu ya ukaguzi lazima ni wizi na ufisadi, wakati mwingine ni ukiukwaji tu wa taratibu. Si kweli kwamba kila hoja ya ukaguzi (audit queries) ya CAG ni ufisadi. Kuna hoja zingine zimeshajibiwa lakini majibu yamepatikana baada ya 'exit meeting', hivyo ripoti hazionyeshi kama kuna majawabu hayo.

Namalizia kwa kutoa wito CAG aongezwe bajeti, afanye udhibiti kabla wizi haujafanyika na tupate ripoti ya udhibiti badala ya ripoti ya ukaguzi pekee.

**Paskali 0754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mbunge Kishimba shahada ya Honoris Causa inamhusu



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

WABUNGE wetu wengi tumekuwa tukiwategemea katika mambo mengi ya kutuwakilisha katika mjengo wa Bunge, yakihusu majimbo yetu lakini pia taifa kwa ujumla wake.

Hivi sasa wako Dodoma wakiendelea na Mkutano wa Bunge la Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, wakijadili mambo makubwa na mazito yanayotuhusu kama wapigakura wao.

Muda ambao pia huutumia kuonekana wanavyotetea maslahi ya wapiga kura wao ili muda mwafaka ukifika wa kurudi bungeni kupitia kura, basi wajitetee kuwa walikuwa wakiwatetea.

Wako wanaotetea wananchi wao kwa namna mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kupayuka na wengine kupangilia masuala yao, wakilenga yaeleweke kwa wahusika ambao ni serikali na hatua mwafaka zichukuliwe.

Miongoni mwa wabunge walionishawishi mpaka niandike hapa, ni Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, ambaye hivi karibuni alisimama akachangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katika alichokizungumza, aligusia pia Ripoti ya ukaguzi wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, akishangazwa na mambo yanavyokwenda nchini hasa katika masuala ya vipaumbele, nini kianze na kipi kifuate.

Kishimba alihoji kwa nini CAG hufanya ukaguzi baada ya fedha kuwa 'zimepigwa' na si kabla ya miradi kuanza? Kwamba wabunge wangekuwa wanashirikishwa wazo la miradi kabla haijaanza, ili kuhakikisha wanasimamia maslahi ya jamii husussan katika fedha!

Akatolea mfano kwamba kwa kawaida mbwa hubweka wakati kuna mwizi ili mwenye mali atoke kupambana naye, lakini akibweka baada ya kuwa wizi umefanyika, ni dhahiri hakuwa eneo la tukio. Yaani CAG asikague baada ya ubadhirifu, upigaji na uhujumu kuwa umefanyika!

Akahoji iweje badala ya serikali kujenga masoko ya bei mbaya kwa matarajio ya watu kwenda kununua nyanya, ingejenga masoko madogo tu yatumiwayo na wachuuzi na wanunuzi kwani kufanya hivyo, kumesababisha masoko kukosa wateja.

Kana kwamba haitoshi, madaktari chungu nzima wanahitimu vyuo na kurudi mitaani kutafuta kazi pamoja na usomi wao wakijaribu kuanzisha vijizahanati vyao na kudunga watu sindano inakuwa taabu, lakini mjasiriamali Mmasai, anauza dawa mtaani tena akiwa na kibali cha serikali.

Mmasai huyo kwa mujibu wa Kishimba, pengine na watu wengine, anakuwa na uhalali wa kutoa mwongozo wa utumiaji dawa hizo, zenye uwezo wa kutibu magonjwa mengi! Tatizo hapo sasa, msomi mtaalamu ananyimwa kibali lakini Mmasai asiye na shule anapata!

Kishimba hakika alikumbusha jinsi Mzee yule au Babu wa Kikombe cha Loliondo alivyonywesha watu dawa zisizo na vipimo kwa imani ya kuponya magonjwa mengi lakini akaachwa aendelee na baadhi ya waliochomoa madripu hospitalini, wakaenda kufia huko.

Kikombe hakikuchagua wala kubagua, kila aliyekuwa na usafiri, alifika kubugia kikombe chake hata waliokuja kuwa marais wa nchi zao baadaye walifanya hivyo, wakiamini dawa za jadi zina nguvu kuliko za kisasa.

Kwa kifupi, Kishimba alitaka kuuambia umma, jinsi nchi inavyoliwa kutokana na mipango ambayo pengine inashindikana kusimamiwa vema na watendaji ambao wanadhani wamefikia hatua ya kumlazimisha Rais Samia Suluhu Hassan kubungua bongo kwa ajili yao.

Si mara ya kwanza mbunge huyu anatoa maoni mujarab yaliyojaa hekima na mwongozo kwa taifa, lakini yawezekana ama anapuuzwa au haijafika siku yake ya kukubaliwa kuwa na mchango mkubwa na adhimu kwa jamii ya Watanzania.

Amekuwa mara nyingi akizungumzia masuala ya elimu nchini na jinsi inavyotakiwa kuendeshwa kwa faida ya kila Mtanzania, pengine hajasikika sawasawa, sina uhakika ni nini sababu, lakini yawezekana ni watu kutofahamu msimamo wake na pengine kueneza elimu aliyo nayo.

Ifahamike, kuwa Kishimba si msomi wa kiwango hicho lakini ana mchango mkubwa usiohitaji vyeti vya darasani ndiyo maana kwangu mimi, namwona kama mtu anayestahili Shahada ya Udaktari wa Heshima (shahada ya uzamivu), yaani Honoris Causa.

Ni vizuri michango kama hii ikaenziwa na kupewa nafasi kwa ajili ya kuikomboa jamii yetu ambayo si ajabu ikapitia kipindi kigumu, kutokana na ugumu wa wahafidhina walioopo wanaotaka kumkwamisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mipango yake ya kuwasaidia Watanzania kutibu makovu yao.

Hili la CAG ambalo sasa limehamishiwa Novemba kujadiliwa na Bunge, tusilichezee kwani Watanzania tunataka kuona wanaokwamisha nchi wanachukuliwa hatua stahiki na tena kali ili mtoto aliyechezea moto aunguzwe sawia.

**Alamsiki!**

## ICCR yafadhili masomo kwa Watanzania 400

Na Romana Mallya

MKURUGENZI wa Kituo cha Utamaduni wa India Swami Vivekananda (SVCC), Dk. Soumya Chavan amesema zaidi ya wanafunzi 400 kutoka Tanzania wamenufaika na ufadhili wa masomo kupitia Baraza la Utamaduni na Uhusiano la India (ICCR).

Aidha, amesema wanafunzi wanaopenda kujiendeleza na masomo ya Shahada, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu katika Vyuo Vikuu vya India kwa mwaka wa masomo 2023/24 kupitia ICCR, watume maombi yao.

Dk. Chavan alisema hayo wakati wa maadhimisho ya miaka 74, tangu kuanzishwa kwa ICCR na kuwataka wale wanaopenda kujiunga na masomo hayo watume maombi kupitia tovuti ya udhamini ya ICCR'S A2A http://a2ascholarships.iccr.gov.in kabla ya Aprili 30, mwaka huu.

Mkurugenzi huyo aliwaomba wanafunzi wakitanzania watumie fursa hiyo ili kupata elimu bora na kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na India katika sekta ya elimu.

Alisema umri wa waombaji wa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Udaktari (PhD) kikomo chake ni miaka 45 na masomo mengine ni kati ya miaka 18 hadi 30.

Alisema waombaji wanaweza kuomba kwa kuchagua vyuo vikuu au taasisi tano kwa utaratibu wa upendeleo wao wa masomo.

Alisema mpaka sasa ICCR ina vituo vya utamaduni 36 ulimwenguni vinavyofanya kazi kupitia ubalozi na wakurugenzi wa vituo vya utamaduni wa India.

# Ulega: Vituo atamizi fursa ya ajira kwa vijana

Na Mbaraka Kambona

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema wizara imeanzisha vituo atamizi vya kuwafundisha vijana ufugaji wa kisasa wa mifugo na samaki lengo likiwa kujibu changamoto za ajira kwa vijana nchini.

Waziri Ulega aliyasema hayo juzi katika Kongamano la Tisa la Wadau wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuhusu masuala ya sera linalofanyika jijini Dodoma kuanzia juzi.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kuanzisha programu hii kwa ajili ya kuandaa vijana kufanya ufugaji wa kibiashara. Kwa mwaka huu tumeanzisha vituo atamizi nane (8) vya kuwafundisha vijana ufugaji kwa tija", alisema.

Ulega alisema kila mwaka takriban vijana 1,600 wanahitimu ngazi mbalimbali za elimu katika vyuo vya mifugo na kati ya hao 150 pekee ndio hupata nafasi katika mfumo rasmi wa ajira, hivyo lengo la ubunifu huo ni kuwezesha vijana wanaobaki nje ya mfumo rasmi wa ajira kujiajiri kupitia unenepeshaji na uuzaji wa mifugo yao ndani na nje ya nchi.

"Mipango yetu katika mwaka wa fedha wa 2023/24 ni kuwa na vituo atamizi 30 ambavyo vitakuwa na vijana wasiopungua 30 na kutufanya kuwa na vijana 900 ambao watakuwa wamepata mafunzo na hivyo kusaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa ajira hapa nchini ",alisema.

Waziri aliongeza kuwa tayari wizara imeshatafuta masoko kwa ajili ya vijana hao kuuza mifugo yao na kwa mwaka vijana hao watauza mifugo yao takriban mara nne kwa mwaka, hivyo kuwawezesha kupata kipato ambacho kitawasaidia kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo.

Pia alisema vituo atamizi hivyo wamevianzisha pia kwa upande wa sekta ya uvuvi kwa ajili ya vijana kuboresha ujuzi wa ufugaji wa samaki na uvuvi.

Kaulimbiu na dhima ya kongamano hilo ni: "Ushindani wa Tanzania Katika Soko Huru Barani Afrika (AfCFTA): Changamoto na Fursa Katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".




Mkurugenzi wa Taasisi ya Al-HEKMA, Shekhe Nurdeen Kishki (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kutoa shukrani zake kwa Watanzania kushiriki kikamilifu katika mashindano ya Qur-aan Afrika yaliyofanyika hivi karibuni, pia ametangaza kudhamini vijana 50 wanaohitaji kufunga kushoto ni Katibu Mkuu wa Mashindano ya Qur-aan wa Taasisi hiyo, Salum Kiza. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Kazi za washindi uandishi bunifu kusambazwa nchini

Na Halfani Chusi

WAZIRI wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof Adolf Mkenda, amewaahidi washindi wa tuzo ya taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu, kuwasaidia kuchapisha kazi zao na kuzitawanya nchi nzima ikiwamo shuleni.

Mkenda alitoa ahadi hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa utoaji wa tuzo hizo iliyohudhuriwa na viongozi wa ndani na nje ya nchi akiwamo Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Msumbiji, Joaquim Chissano.

Mkenda alisema washindi waliopatikana kwenye kinyang'anyiro hicho, wameliheshimisha taifa na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

"Washindi waliopatikana leo, kwenye uandishi bora wa Riwaya na Ushairi, kazi zao zitasambazwa nchi nzima ili kila Mtanzania aweze kupata na kusoma kazi nzuri zilizowasilishwa.

"Tutavipeleka hadi kwenye shule zetu ili wanafunzi waweze kusoma, kwa sababu kusoma vitabu kunajenga afya ya akili hivyo, niwaombe Watanzania tujenge utamaduni wa kusoma vitabu" alisisitiza.

Rais Mstaafu Chissano ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo, aliipongeza serikali kwa kuandaa tuzo hizo, na kusema kwamba imetambua na kuthamini lugha ya Kiswahili nchini na Afrika kwa ujumla.

"Lugha ya Kiswahili, ipo rasmi Umoja wa Afrika (AU) na inazungumzwa takribani katika mabara yote, niwapongeze Watanzania kwa kutambua na kuenzi mchango wa Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere kwa kukuza lugha hiyo.

"Ni wazi kabisa aliikuza kwa kuandika maandiko bunifu kama mashairi, riwaya, na kutafsiri kazi mbalimbali za fasihi ya Kingereza kwa Kiswahili ni heshima kubwa tuzo hii kupewa jina lake" alisifu.

Alishauri juhudi hizo ziendelee bila ukomo na kusema kwamba, uhai wa lugha yoyote duniani ni pamoja na kuwapo kwa machapisho yaliyo andikwa kwa lugha yake.

"Kiswahili ni lugha yetu Afrika, hatuna budi kukilinda na kukikuza kwa kukipa heshima na dhima mbalimbali mathalani kutumika katika elimu, siasa utawala na masuala mengine ya kijamii" alisema Rais huyo ambaye ni maarufu kwa kutumia Kiswahili kwenye mikutano ya kimataifa.

Tuzo hizo zilitolewa kwa washindi 10 katika kipengele cha mwandishi bora wa mswaada wa riwaya na ushairi, ambapo mshindi wa kwanza mpaka wa tatu alikabidhiwa tuzo hiyo na Rais Mstaafu wa Msumbiji.

Kwenye kipengele cha muandishi bora wa mswaada wa riwaya, Hamisi Kibari kutoka Dar es Salaam aliibuka mshindi wa kwanza na kupata zawadi ya Sh.milioni 10, ngao na cheti.

Rikson Mtare kutoka Dar es Salaam, akiibuka mshindi wa pili na kupata zawadi ya cheti na Sh. Milioni saba.

Mshindi wa tatu ni Zainabu Ali Muhamudu kutoka Zanzibar ambaye alipata Sh. milioni tano na cheti. Kwa upande wa ushairi, mshindi wa ni Amri Abdalah, kutoka Kilimanjaro akifuatiwa na Athmani Maulidi kutoka Zanzibar na Sufian Almas kutoka Tanga ambao walipewa zawadi sawa na washindi wa riwaya.

Washindi wengine kutoka nafasi ya tatu mpaka ya kumi walitambuliwa kwa kupewa vyeti.

# MAISHA

APRILI 16, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## Juisi ya tende

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Dondoo za faida uwekezaji wa nyumba




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# ONDOA WEUSI KWAPANI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| L | O | A | | P | E | A |
| I | | | | E | | N |
| P | | G | I | A | | G |
| I | P | O | | N | I | A |
| Z | | N | O | A | | Z |
| I | | G | | | | W |
| A | N | A | | A | D | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MTI, NOA, GOA, INI, PWANI, IBEBE, IAMUE, AMINI, IKWAMUE, TANGANI

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | 8 | 7 | 3 | 5 | 6 | 3 | 7 | 1 | 7 | 3 |
| 8 | 1 | 3 | 8 | 6 | 8 | 5 | 8 | 2 | 6 | 4 |
| 8 | 3 | 7 | 8 | 3 | 9 | 7 | 5 | 8 | 8 | 7 |
| 1 | 9 | 4 | 7 | 6 | 7 | 8 | 9 | 5 | 7 | 8 |
| 1 | 9 | 0 | 4 | 8 | 6 | 7 | 3 | 9 | 5 | 7 |
| 4 | 5 | 6 | 9 | 0 | 4 | 8 | 9 | 8 | 4 | 7 |
| 9 | 9 | 5 | 8 | 7 | 9 | 5 | 7 | 5 | 9 | 5 |




## WATOTO

# PAKA RANGI




CHEKA

KICHEKESHO

HAKUNA watu wenye ndugu wengi kama makonda wa daladala. Ebu msikie konda huyo wa Posta kwenda Makumbusho.

"Haya dada hapo mbele, mjomba kule mwisho kaa vizuri...oyaa mamdogo unaenda? Bibi shuka taratibu, shemeji umeikuta haya panda. Babu njoo ukae! Baba angu hapo tusogee kidogo,"

"Shangazi maliza ngazi,Swaiba geukia mbele, Kaka hapo shika upande wa pili,mdogo wangu mpishe mama mkwe akae,"

Wakimaliza kazi wana ndugu kibao walioonana nao siku moja tu.

**SWALI**

Mawe ya Matambawe yanapatikana sehemu gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Wanawake waliofanya waume kuwakimbia sasa wanavyojuta!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kujadili Maisha ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilirusha swali kwamba 'kwa nini wanandoa waachane kisha waanzishe familia zingine?

Nikatoa mfano msomaji wetu mmoja wa safu hii aliyeelezea uzoefu wake akasema kuwa kwa asilimia kubwa ya wanaume wanaozikimbia nyumba zao na kuanzisha ndoa zingine wanasukumwa na mambo kadhaa.

Moja akataja kupanda gharama za maisha huku kipato kikishuka. Pili, kutokuwa makini wakati wa kuchangua mwenza wa kuishi naye katika ndoa. Hapa inawezekana ni uchumba kuwa wa muda mfupi kabla ya kufahamiana kwa undani. Hizi tunaita ndoa za utotoni. Baadaye wanagundua kuwa kumbe haikuwa chaguo sahihi.

Msomaji wangu, hebu nikupe mifano mingine kwa nini mwanaume akimbie nyumba yake au mwanamke ahame tena wakati mwingine akiacha watoto nyuma kuepusha balaa zaidi.

Baada ya kusoma makala ya wiki iliyopita, baba mmoja akatuma ujumbe ufuatao kupitia simu ya kiganjani. Akasema hivi: "Flora sawa, lakini pia kuna mengi zaidi ya hayo. Kwa mfano, mimi ni mmoja wa wahanga wa hayo matatizo. Mimi ni mzee na babu wa watoto watatu, lakini nilihama niliacha nyumba nikaenda kupanga kwa gubu la mke.

"Baada ya mke kazi kuisha akawa anawatumia watoto nirudi. Nilikataa na kwa bahati nzuri nilishajenga kibanda changu na kuwa na kigari kingine. Ukweli hadi sasa sijaoa na sitaki tena kuoa kwani wa kuniliwaza wapo wengi tu!"

Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia vema mwenzetu huyu. Mwanaume ni kiongozi wa familia, ni kichwa cha nyumba. Mwanaume ndiye anayepepesa macho kuchagua yule ampendaye na kumtolea mahari ili amkaribishe kwenye himaya yake.

Ndiye anayeanza kumvisha pete ya uchumba mwanamke na kisha pete ya ndoa kumkaribisha katika maisha ya ndoa. Sasa unapoona mwanaume aliyemuingiza mwanamke nyumbani kwake akitarajia maisha mazuri yaliyosheheni upendo, furaha, amani na utulivu anaikimbia nyumba yake, ujue mambo ni magumu!

Baba huyu kwenye ujumbe wake hakutaka kuingia kwa undani yale aliyofanyiwa na mkewe hata kukimbia, kwa hekima akayaficha lakini akaona taratibu aondoke zake kutafuta amani ya moyo na pengine kunusuru maisha yake.

Pengine angeendelea kukaa ghadhabu ingempata na kufanya kitu kibaya ambacho kingegharimu maisha yake na wengine ndani ya familia yake. Inavyoonekana anayo amani na maisha yanaendelea.

Akasema kwenye ujumbe wake kwamba, mwanamke kazi ilipoisha akaanza kummisi mumewe na kuwatumia watoto wambembeleze arudi nyumbani.

Swali, je, kile kilichosababisha baba huyu kukimbia nyumba yake kimerekebishwa? Na je, usalama wake akirudi utakuwaje? Na je, hapo alipo baba huyu anakosa nini? Kama alisimangwa na gari au nyumba, vyote hivi kwa sasa anavyo, tena na amani juu.

Mama huyo wakati akiwa kazini alijiona na kumdharau mume wakati akidhani kuwa kazi ile isingeisha siku moja. Sasa anatumia watoto kumbembeleza baba yao arudi nyumbani. Kwa nini yeye asifanye hivyo? Pengine ni aibu akikumbuka vitimbwi alivyomfanyia awali. Sasa yuko nyumbani kivuli cha mume wake kinamtesa hadi kuwasumbua watoto wamrejeshe baba yao. Kwani wao ndio waliomfukufa?

Msomaji wangu, wanawake wengi ambao wako kwenye mamlaka ndoa zao ziko kwenye sintofahamu nyingi. Wengine hata huko majumbani mwao kila mmoja analala chumba chake, walishatengana kitambo, bora maisha yaendelee. Na hawa wengine wana mahusiano mengine huko nje.

Maisha yanapofikia hatua watoto ndio wanakuwa wasuluhishi wa migogoro ya wazazi wao, ujue hizo familia zinapitia magumu. Lazima wazazi wenyewe watafute chanzo cha wanayopitia.

Wakati mwingine yanatokana na chimbuko au asili yao. Warudi nyuma kutafuta linalowapata leo, je, limekuweko huko walikotoka?

Ieleweke pia kwamba si wanaume tu huzikimbia nyumba zao pale mambo yanapokuwa hayaendi. Tena wanawake ndio wakimbiaji wazuri na ili kujihami hukimbilia mahakamani pale ushahidi wa kutosha unapokuwa dhahiri.

WaKo wanaokimbia vipigo vya waume zao, waume kuwaletea hawara nyumbani ili wasome upepo kwamba wamechokwa, wanaume kuwa walevi huku matumizi nyumbani hayaonekani na kadhalika.

Mjadala huu ni mpana tuangalie muda mwingine baadaye tuchambue kwa kina. Ama kweli Maisha Ndivyo yalivyo.

***Una kisa? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kwa hili TANESCO, mna cha kuwajibu Watanzania

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22, imekuja na sura mbili tofauti kuhusu utendaji na ufanisi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kwa kuwa sasa ni ruksa kwa umma kuisoma ili kujua kilichomo ndani yake, ni dhahiri kwamba shirika linapaswa kutoa majibu yake kwa Watanzania.

Kwa wasiokumbuka au walipitiwa ni kwamba ripoti hiyo ya CAG ilianza kuwa wazi Aprili 5, mwaka huu, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kutimiza matakwa ya Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Tanzania kwa kuiwasilisha Bungeni, jijini Dodoma ikiwa na ripoti 22.

Baada ya kuwasilishwa kwake, mwandishi wa waraka huu ni miongoni mwa waliobahatika kuisoma na kuona upungufu ambao CAG amebaini.

Jambo la kwanza, TANESCO inapaswa kujibu kuhusu kutokuwapo kwa udhibiti wa kutosha wa upotevu wa nishati, ufanisi mdogo katika kutumia rasilimali na changamoto zingine zinazohitaji kutatuliwa ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wenu unafikiwa.

Pili, ni suala la ugumu wa kufuatilia usomaji wa mita kwa mitambo ya kulisha umeme na usambazaji wa umeme (ikiwa ni pamoja na watumiaji wakubwa wa nishati) kutokana na upungufu wa maelezo kuhusu mitambo ya kulisha umeme au vituo vidogo vya umeme katika mfumo wa usomaji mita moja kwa moja.

Jambo la tatu ni la mita za umeme 874,019 kutothibitishwa na Wakala wa Vipimo (WMA). Katika mwaka wa fedha 2021/22, TANESCO ilinunua na kutumia mita 874,019 zenye thamani ya Sh. bilioni 115, lakini hazikuthibitishwa na WMA, kitu ambacho kinaweza kusababisha hasara kwa mteja au shirika.

Kimsingi, ni hoja ambazo zisipojibiwa kwa weledi zitaendelea kuacha ukakasi kwa Watanzania kuhusu shirika lao. Ingawa kwa miaka kadhaa sasa, serikali imekuwa ikichukua hatua muhimu za kuendeleza miundombinu yake na kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wake.

Katika pitia yangu ya ripoti ya CAG, nimeona amebaini upungufu ambao ni wa mfumo wa kufuatilia upotevu wa nishati ya umeme, mita na vifaa vinavyotumika kupima nguvu inayosambazwa kutoka kwenye kituo ambacho umeme unapokelewa kutoka kiwanda cha uzalishaji.

Katika ripoti hiyo, CAG ameeleza laini ya umeme ni mtandao wa kuhamisha nishati kutoka vyanzo vya umeme hadi kwenye vituo vya usambazaji au watumiaji. Lakini mapitio yake ya mita katika laini za umeme, yalibaini kati ya mita 1,803 za vituo vya umeme vilivyopo katika mikoa 29, taarifa za mita 1,638 (asilimia 90.8) hazikuoneshwa katika mfumo wa usomaji mita moja kwa moja kwa mwaka mzima.

Aidha, mita 52 zilikuwa na usomaji wa nishati iliyopokelewa pekee, wakati mita 80 zilikuwa na usomaji wa nishati iliyosafirishwa pekee; ambapo suala hilo ni kinyume na Kanuni Namba 45 (1) ya Kanuni za Sheria ya Umeme (Huduma za Ugavi) za Mwaka 2019.

Katika uchambuzi wake, CAG ameeleza kuwa uongozi wa shirika ulielezea sababu kuu za udhaifu huo kuwa ni matatizo ya mtandao na mita zilizoharibika kwenye vituo vya umeme.

Kwa maoni yake, ufungaji wa mita katika mitambo ya umeme haukuakisi thamani ya fedha, na kuna uwezekano kuwa baadhi ya mita au mitambo ya umeme imefanyiwa udanganyifu au kughushiwa.

CAG anaona jambo hilo linaweza kusababisha wizi wa nishati unaofanywa na wateja (hasa watumiaji wakubwa wa nishati) kwa kushirikiana na wafanyakazi wasio waaminifu.

Kutokana na upungufu huo, CAG amependekeza TANESCO itekeleze matakwa ya Kanuni za Uzani na Vipimo za Mwaka 2019, ili kuhakikisha mita zinapimwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo kabla ya kutumiwa na wateja

Kwa uchambuzi huo wa CAG na mapendekezo aliyoyatoa, ninaona kabisa kuna maswali TANESCO inatakiwa kuyajibu kwa Watanzania.

# UTATOKAJE KWENDA KUFUNGA UCHUMBA?









# MITINDO







# NYEUSI NI UTANASHATI

WANAUME wanatakiwa kuwa makini katika kufanya chaguo sahihi la mavazi ili waendane na mazingira ya kisasa.

Tabia za kutojali sana kuchagua nguo zinazolingana na hitaji la mwili wake, inawafanya kutokuwa maridadi kutokana na kuvaa nguo tofauti na mwonekano.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanashauri utanashati wa mtu ni pamoja na umakini wakati wa kununua mavazi.

**JINSI YA KUCHAGUA**

Kama wewe ni mvivu kununua nguo, hakikisha unanunua mavazi ya rangi nyeusi kwa sababu zina kawaida ya kutochagua rangi wala kuchosha muonekano wa mtu.

Mwanaume anapovaa suruali yeusi hahitaji kufikiri sana kuhusu rangi ya shati, viatu au fulana.

Suruali nyeusi haichagui rangi ya vazi au nguo yoyote inayoambatana nayo.

Unashauriwa kuchukua suruali yenye kubana kiasi kwa sababu unapovaa na shati muonekano wako unakuwa wa kipekee.

**VIATU**

Suruali nyeusi inafaa sana kuvaliwa na viatu vya rangi nyeusi, udongo au nyeupe iliyofifia.

Hata hivyo wengine wanapenda kuvalia viatu vya wazi vya rangi yenye mng'aro dhaifu na wanatoka bomba.

## UREMBO
**Na Mary Geofrey**

# ONDOA WEUSI KWAPANI

KUWA na weusi kwenye mapaja na sehemu zingine za mwili ni hali inayoathiri kisaikolojia na kuleta msongo wa mawazo.

Hali hiyo inakunyima uhuru wa mavazi na kujiachia unapokuwa na mwenza wako.

Ndio maana wanawake wengi wamekuwa wakijaribu njia nyingi sana bila mafanikio. Wanafikia hadi kutumia kemikali ambazo zinawaongezea tatizo kuwa sugu zaidi.

**ALOEVERA**

Chukua utomvu wa jani la Aloevera pale pale unapokata. Paka kwenye sehemu yenye weusi na kisha acha ule utomvu kwa muda takribani nusu saa kisha osha na maji ya uvugu vugu/moto. Fanya hivi mara moja hadi mbili kwa siku ili kuweza kupata matokeo haraka. Unaweza pia kutumia

**YOGURT**

Kuna maajabu makubwa sana na yogurt kwani imekuwa ikitumika kama natural bleaching agent kutokana na kiini chake lactic asidi pamoja na zinc yenye uwezo mkubwa wa kuzuia kuharibika kwa ngozi kutokana na jasho jingi sehemu za mapaja, shingoni na kwapa.

Chukua yogurt paka sehemu husika kisha sugua halafu acha kwa dakika 10-15 na baada ya hapo osha na maji ya uvugu vugu.

**LIMAO**

Limao ina asili ya tindikali ambayo inafanya itumike kama kisafisha ngozi yako ambayo imeharibika.

Pia limao ina kiwango kingi cha vitamin C kinachosaidia seli za ngozi yako kuzalishwa upya na kasi ya ajabu.

Chukua pamba na chovya kwenye juisi ya limao kisha paka sehemu husika kisha acha kwa dakika 20 baada ya hapo osha na maji masafi.

**TANGO**

Hii pia imekuwa ikishika nafasi kubwa kama ni natural bleaching agent ya ngozi. Ina uwezo mkubwa wa kuondoa seli za ngozi zilizokufa na kurudisha mpya haraka sana. Na hatimaye kufanya mapaja yako kuwa meupe na sehemu zingine.

Chukua kipande cha tango au juisi yake sugua sehemu husika kwa dakika 10 hadi 15. Kisha acha angalau dakika 10 tena baada ya hapo osha kwa maji ya uvugu vugu.



## MAPISHI
**Na Mary Geofrey**



# Juisi ya tende

JUISI ina faida nyingi katika mwili wa binadamu, zipo juisi za aina mbalimbali ambazo zinatokana na mimea na mizizi aliyoumba Mungu.

Juisi ya tende ni miongoni mwa juisi zilizojizolea umaarufu mkubwa hasa katika kurekebisha tatizo la nguvu za kiume.

Mahitaji

Tende kilo moja, maziwa ya unga au ya ng'ombe lita moja, sukari kiasi upendacho. Zingatia kuwa tende zina asili ya sukari hivyo hakikisha unaweka kiasi.

Namna ya kutengeneza

Chukua tende zako kisha zitoe mbegu zake, hakikisha unatoa mbegu tu na kuziacha tende kama zilivyo bila kutoa kitu kingine.

Anza kuzisaga peke yake kwenye brenda hadi zitakapolainika sawasawa.

Mimina maziwa yako kidogokidogo kwenye brenda ili kuzisaga vema jambo litakalosaidia juisi yako kulainika vema.

Baada ya kutia maziwa yote na kuisaga sawasawa, tia sukari kiasi upendacho huku ukiendelea kuisaga ili sukari yako iweze kuchanganyika vizuri na juisi yako.

Juisi yako itakuwa tayari kwa kunywa sambamba na kitafunwa chochote ukipendacho kama vile bagia, sambusa, korosho au karanga au hata baada ya kupata futari yako.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya




# DONDOO ZA FAIDA UWEKEZAJI WA NYUMBA

UJENZI wa nyumba ni miongoni mwa eneo muhimu linalotumiwa na wengi kuwekeza.

Uwekezaji ni mchakato mzima wa kuiweka mali katika mfumo maalum wa kifedha kwa ajili ya tija zaidi ya baadae ambayo inaweza kuongezeka au namna fulani yenye kuleta faida baada ya muda fulani.

Leonald Michal, yeye ni mshauri wa masuala ya uwekezaji, anaelezea kanuni bora za kuwekeza kwa tija. Anashauri kwamba unapowekeza kwenye ujenzi wa nyumba miongoni wa mambo ya kuzingatia ni pamoja na unataka kujenga nini kulingana na mahitaji katika uhalisia wa sasa na wa baadae.

"Kutazama ni aina gani ya watu watakaotumia nyumba yako, shughuli gani ambazo zitakuwa zinafanyika katika nyumba husika.Kwa hiyo ni muhimu pia kushirikiana na mtaalamu aliyebobea katika usanifu.

"Pia kujenga kwa kuzidi uwezo wako huleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi, sehemu nyingine kutotumika na kutokuwa na faida ya kutosha, kutumia pesa nyingi kwa kitu kisicho na faida na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji wa jengo," anasema.

"Kujenga kwa kutokidhi mahitaji, husababisha hasara kwa kulazimika kufanya upanuzi wenye gharama kubwa zaidi, kuacha nyumba na kutafuta nyingine, kutoridhika na kutokuwa huru zaidi.Ni muhimu kuhakikisha kwamba unachojenga kitaleta faida kwa kipindi hicho cha uwekezaji," anasisitiza.

Anashauri kwamba ni vyema kujiuliza maswali kama je kodi ambayo wapangaji wanailipa inaleta faida, mtaji uliotumia kujengea utakuja kujilipa baada ya muda gani, faida ya kipesa itaanza kupatikana baada ya muda gani, na je nyumba yako itadumu kwa miaka mingapi?

Jambo lingine muhimu, anasema unapowekeza katika sekta hiyo ya nyumba ni kufuata sheria na taratibu zote husika ili uwekezaji wako usibughudhiwe na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuhatarisha mchakato wa kupata faida kwa kujenga katika eneo linaloruhusiwa kisheria na kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Makadirio ya gharama za ujenzi yatakusaidia namna ya kujipanga juu ya mtaji wa kukuwezesha kusogeza mbele na kazi yako na kwamba si vyema kujenga kwa kubahatisha.

"Ni muhimu kuiona faida katika mipango yako ambayo umeifanya kabla ya kuanza ujenzi," anasema.



## Zingatia haya kuifurahia nyumba yako

Na Restuta James

TASNIA ya mitindo na mapambo ya nyumba inaendelea kukua kwa kiwango cha juu kuanzia ramani ya nyumba, ujenzi wake, rangi hadi samani.

Hata hivyo, maeneo hayo makuu ya kuangalia wakati na baada ya ujenzi nayo yamegawanywa na wanatasnia ya mapambo wanachambua mpangilio wa rangi za sebule, jikoni, vyumba vya watoto, chumba kikuu (master bedroom), vyoo hadi bustani.

Ni vigumu katika makala moja kuchambua maeneo yote japokuwa leo ninaweza kukudokeza kwamba wataalamu wa mapambo ya nyumba, wametaja rangi ya bluu tulivu (tranquil blue), ndiyo inayoshika namba moja kwa mwaka huu.

Wanaeleza kwamba ni rangi inayosababisha utulivu na kwamba inafaa kupaka katika maeneo mengi husani sebuleni, ofisi na sehemu za kufanyia ibada.

Pamoja na rangi hiyo, wataalamu wa mapambo wametaja mambo ya kuzingatia ili uweze kuifurahia nyumba yako.

1. **Nunua samani zenye droo**

Wataalamu hawa wanaeleza kwamba ili chumba au nyumba iwe na mpangilio mzuri, ni muhimu kununua samani ambazo zina sehemu ya kuhifadhia vitu, ili uweze kuweka kila kitu kwenye mpangilio.


Wanatoa mfano kwamba, kama unaishi kwenye nyumba ndogo, unaweza kununua 'kochi kitanda' kinachoweza kutumika pia kama kabati.

Wanaeleza hii itakusaidia kutumia nafasi ndogo vizuri na ikaonekana nadhifu kwa kuwa mchana unatumia chumba chako kama sebule na usiku ni chumba cha kulala.

Jambo lingine wanalotaja wataalamu hawa ni taa na rangi.

Wanashauri kwamba ukubwa au udogo wa chumba ndio utaamua uweke taa za aina gani na wapi. Wanasema kwa ujumla, chumba chochote kinahitaji mwanga wa kutosha ili kuongeza nakshi; japokuwa kuna mazingira yatakulazimu uweke mwanga hafifu kama mishumaa au taa za rangi kulingana na hitaji lako.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
DUH! KUMBE KAMA MFUKONI 'EMTE' KIDALI KINAGEUKA ZIGO!
JUKWAANI
NIKIKANDAMIZA HILI, KASWAUMU KANAKUWA KAMSELELEKO
'DAKU'
WEWE NIONGEZE ALAFU YA HUKO MTAANI NIACHIE MWENYEWE SITOKUAIBISHA
MWEZI HUU WENZAKO WANAKUJA 'KISAILENSA' WANATOA LOKI WANAONDOKA BILA KELELE!
GONGO
MUME WANGU NISHAZOEA UNANIACHIAGA 'BUKU TATU' ZA FUTARI, SASA LEO UMEACHA BUKU KUMI NA TANO!
MASAJI SPESHO
USHANIUMIZA NA FUTARI YAKO YA KIHUJUMU UCHUMI. 'CAG' AJE TU
WE'HUJUI KAMA WATU TUMIFUNGA SHETWANI WE! EMBU TAJA NAMBA NAIKARIRI
NAMBA NDIO HIYO ISOME TU
WATOTO HAWA NILOWAZAA KAMA NILIAHIDIWA TUZO KADRI IDI INAVYOSOGEA SUKARI PRESHA NAVYO VINAZIDI KUSOGEA JUU...
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SAKO LA NYANI NGEDERE HAPONI...

## Waziri mkuu atupiwa bomu la machozi

**TOKYO,** JAPAN

WAZIRI Mkuu wa Japan Fumio Kishida ameondolewa haraka baada ya bomu la machozi kutupwa katika mkutano wa hadhara.

Mtu mmoja alizuiliwa katika eneo la Wakayama, ambako Kishida alipaswa kutoa hotuba, vyombo vya habari vya ndani viliripoti.

Shuhuda mmoja alisema waliona mtu akirusha kitu, na kufuatiwa na moshi, huku mwingine akisema walisikia kishindo kikubwa.

Picha zilionyesha maafisa wakirundikana juu ya mtu anayeaminika kuwa mshukiwa.

Polisi walisema wamemkamata.

Shirika la utangazaji la umma la Japan [NHK } lilionyesha kanda zilizoonekana kuonyesha umati wa watu wakikimbia kutoka eneo la tukio.

Kishida alikuwa ndio kwanza ameanza kutoa hotuba baada ya kuzuru bandari ya wavuvi huko Wakayama kifaa hicho kiliporushwa na kujifinika kuashiria kujikinga, NHK iliripoti.

Tukio hilo linawadia baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu Shinzo Abe kuuawa kwa kupigwa risasi akiwa kwenye kampeni mwaka jana

**BBC**

## China yasisitiza Taiwan sehemu yake

**BEIJING,** CHINA

CHINA imepinga vikali uingiliaji wowote wa kigeni juu ya suala la hadhi ya kisiwa cha Taiwan na kuyahimiza mataifa mengine kuheshimu msingi unaotambulika kimataifa wa Taifa moja.

Waziri wa mambo ya kigeni wa China Qin Gang, amewaambia waandishi wa habari mjini Beijing kuwa Taiwan ni sehemu ya China na taifa hilo halitaruhusu nguvu kutoka nje kubadili ukweli huo.

Gang alikuwa akizungumza baada ya kukutana na waziri wa mambo ya nje wa Ujerumani Annalena Baerbock anayeitembelea China tangu juzi.

Akiwa nchini humo Baerbock a lisisitiza kwamba Ujerumani inazingatia "Sera ya China moja" lakini hakusita kugusia mvutano unaendelea sasa kwenye ujia wa bahari wa Taiwan na kuhimiza umuhimu wa kutulizwa mzozo uliopo kwa njia ya amani.

**DW**

## Mtu aliyevujisha siri za Marekani afikishwa kortini

**WASHINGTON,** MAREKANI

KIJANA aliyekamatwa na vyombo vya usalama vya Marekani akishukiwa kwa uvujishaji mkubwa wa nyaraka za siri amepandishwa kizimbani na kusomewa mashtaka ya jinai yanayomkabili

Jack Teixeira mwenye umri wa miaka 21 na mfanyakazi wa kamandi ya kikosi cha ulinzi wa anga ya Marekani, alikamatwa juzi Alhamisi baada ya wiki nzima ya uchunguzi juu ya kuvuja kwa nyaraka nyingi za siri ikiwemo kuhusu vita vinavyoendelea nchini Ukraine.

Wizara ya Sheria ya Marekani inatazamiwa kuainisha kesi ya jinai inayomkabili na kumfungulia mashtaka chini ya sheria ya ujasusi inayoainisha kuwa ni kosa kuvujisha taarifa za ulinzi wa taifa.

Waendesha mashtaka wanaamini kijana huyo ambaye pia ni mtaalamu wa teknolojia alikuwa kiongozi wa kundi la mawasiliano kwenye mtandao ambako nyaraka hizo za siri zilisambazwa

**DW.**

# Watu wanane wauawa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

WATU wanane akiwemo mtoto wa umri wa miaka miwili wameuawa katika shambulio la makombora ya Russia katika eneo la Sloyansk , katika mkoa wa Donbas mashariki mwa Ukraine.

Gavana Pavlo Kyrylenko alisema watu wengine karibu 21 wamejeruhiwa katika shambulio hilo lililofanyika kwenye mji wa makazi ya raia.

Aliongeza kuwa watu wengine saba hawajulikani waliko, akionya kuwa wanaweza kuwa wamenaswa chini ya vifusi. Katika chapisho kwenye mtandao wa kijamii, Rais Volodymyr Zelensky alilaani kile alichokiita shambulio la kikatili na ovu.

"Hali ya uovu kwa mara nyingine tena inajitokeza," aliandika kwenye Telegram.

'Aliongeza " haitavumilika kuua tu watu mchana kweupe, kuharibu maisha ya watu."

Ofisi ya mwendesha mashtaka ilisema mmoja wa waliouawa ni mtoto wa miaka miwili.

Mshauri mkuu wa Zelensky alisema mtoto huyo alitolewa akiwa hai kutoka kwenye vifusi, lakini alifariki kwenye gari la wagonjwa alipokuwa akipelekwa hospitalini.

Gavana Kyrylenko alisema nyumba tano na vyumba vitano vya ghorofa viliathiriwa katika shambulizi hilo, huku biashara na maduka pia yakiharibiwa katika milipuko hiyo iliyotokea mwendo wa saa 18:00 kwa saa za huko.

Aliongeza kuwa huenda shambulizi hilo lilifanywa kwa kutumia makombora ya S-300.

Mfumo huo hapo awali uliundwa kama mfumo wa ulinzi wa ardhi hadi angani, lakini Russia imezidi kuutumia kufikia malengo ya ardhini nchini Ukraine huku vita vikiendelea na ghala za silaha zimepungua.

Waandishi wa habari kutoka shirika la habari la AFP walishuhudia waokoaji wakichimba kuwatafuta manusura katika eneo la milipuko, huku moshi mweusi ukifuka kutoka kwa jengo jingine kando ya barabara hiyo.

Waliongeza kuwa mtaa huo unaojumuisha uwanja wa michezo ulikuwa umejaa uchafu uliojumuisha kurasa zilizochanika kutoka kwenye vitabu vya shule na michoro ya watoto.

Hapo awali, Andriy Yermak mkuu wa ofisi ya kibinafsi ya Zelensky - alisema milipuko saba imesikika katika jiji hilo, ambayo baadhi ilifanyika karibu na shule.

Wakati Ukraine bado inadhibiti Sloyansk, mji huo uko umbali wa maili 27 kaskazini-magharibi mwa Bakhmut, ambao umekuwa kitovu cha mashambulio makubwa ya Russia kwa miezi kadhaa.



Jengo lililoteketezwa na makombora katika shambulio lililofanywa na Russia katika eneo la Sloyansk katika mkoa wa Donbas nchini Ukraine jana. **PICHA: AFP**

# Serikali, waasi wabadilishana wafungwa

**SANAA,** YEMEN

KUMEFANYIKA mabadilishano ya wafungwa kati ya pande zinazozozana nchini Yemen ambayo yanaonekana kama sehemu ya juhudi za kumaliza mzozo wa miaka minane.

Maafisa wa Msalaba Mwekundu walisema wafungwa 318 wamesafirishwa kwa ndege nne kati ya mji mkuu unaoshikiliwa na waasi, Sanaa hadi mji wa Aden unaoshikiliwa na serikali.

Takriban wafungwa 900 wanatarajiwa kubadilishana kwa muda wa siku tatu zijazo.

Vita kati ya waasi na vikosi vinavyoiunga mkono serikali vinavyoongozwa na Saudia vimesababisha vifo vya maelfu ya raia wa Yemen.

Pia imezua kile ambacho Umoja wa Mataifa umekiita mojawapo ya majanga mabaya zaidi ya kibinadamu duniani, huku baadhi ya asilimia 80 ya raia wakilazimika kutegemea chakula cha msaada ili kuishi.

Mabadilishano hayo makubwa zaidi tangu mwishoni mwa mwaka 2020 yanaonekana kama hatua ya kujenga imani, kufuatia mazungumzo mapema wiki hii mjini Sanaa kati ya ujumbe wa Saudia na waasi wa Houthi yenye lengo la kufikia usitishaji vita na unaoweza kuwa wa kudumu.

Mazungumzo hayo yaliwezeshwa na Oman, ambayo inashiriki mpaka na Saudi Arabia na Yemen na imekuwa na jukumu muhimu katika majaribio ya kumaliza mapigano kwa miaka.

Kumeongezeka kasi ya kumaliza vita tangu Saudi Arabia na Houthis kuanza tena mazungumzo ya moja kwa moja mwaka jana. Matumaini yalizidishwa wakati Saudi Arabia na hasimu wake mkuu Iran muungaji mkono mkuu wa Wahouthi walikubali mwezi uliopita kurejesha uhusiano baada ya mzozo wa miaka saba.

Licha ya kushindwa kukubaliana kuendelea na usitishaji mapigano wa miezi sita uliosimamiwa na Umoja wa Mataifa mwezi Oktoba, kumekuwa na kupungua kwa kasi kwa mapigano, ikiambatana na baadhi ya hatua za kupunguza hali ya wasiwasi.

Pia kuna hatua ya kurahisisha vizuizi vya uagizaji bidhaa na kubadilishana wafungwa, iliyokubaliwa katika mazungumzo yaliyofanyika nchini Uswizi mwezi Uliopita.

**BBC**

## MAKALA

# FIKRA ZINAZOKWAMISHA MAENDELEO YA VIJANA



Na Magabilo Masambu

KAMA mtakumbuka, mwaka jana yuko kijana mmoja aliyekuwa mtumishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) mjini Mbeya alimuua baba yake mzazi kwa madai kwamba hakumwandalia maisha. Kwa mtazamo wake aliona baba yake alipaswa kumpa maisha zaidi ya yale aliyokuwa nayo.

Wako watu walichukulia kitendo hicho kama afya ya akili lakini mawazo kama haya yana vijana wengi na baadhi ya watu wazima wanaolalamika kwamba baba zao hawakuwasaidia.

Wengine ni wasomi na hawajioni katika nafasi ya kubadilisha maisha yao na ya familia zao wakiwemo wazazi wao.

Pili, ni kuhusu jambo la kushikwa mkono.

Vijana tulio wengi imani tuliyo nayo ambayo imetupoteza na kutupotosha sana ni kudhani kwamba kila aliyefanikiwa alishikwa mkono.

Tunaamini sana katika kitu kinaitwa 'connection' lakini wakati unahitaji kushikwa mkono una nini mkononi mwako? Katika kitabu cha Kutoka sura ya nne kuna habari juu ya Musa kuhusu fimbo aliyokuwa nayo mkononi baada ya kuulizwa na Mungu ana nini.

Musa akajibu: "Lakini tazama hawataniamini wala hawataisikia sauti yangu maana watasema Bwana hakukutokea" lakini Bwana alimwambia

"Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?" Akasema ni fimbo, akamwambia itupe chini akaitupa nayo ikawa nyoka Musa akakimbia mbele yake.

Bwana akamwambia "Musa nyoosha mkono wako kamshike mkia" akaunyoosha mkono wake akamshika naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake.

Tazama, Musa hakuwa anajua thamani ya fimbo aliyokuwa nayo mkononi na hakuwa na imani kwamba watu wangemwamini kupitia fimbo hiyo.

Maana yake alipokuwa mbele yao ili kuwahakikishia kwamba Mungu alimtokea ni kufanya hiyo miujiza ya kutupa fimbo chini kugeuka nyoka na kurudi kuwa fimbo.

Je, unajua nini ulicho nacho mkononi mwako? Kama unakijua, unajua thamani yake? Je, ulicho nacho umewaonyesha watu? Unajua kwamba ulicho nacho ndiyo muujiza wako?

Kwa lugha rahisi, una nini kitakachoweza kukutambulisha kwa watu au unataka wewe ndiyo ujitambulishe kwao? Kwa nini Mungu alimwuliza Musa una nini na hakumuuliza wewe ni nani?

Nina mfano wa kijana aliyemaliza chuo kikuu mwaka 2014, katika masomo ya Baiolojia na Kemia. Mwaka jana alinitafuta nimtafutie kazi, nikamuuliza umewahi kufundisha kokote?

Akasema hajawahi ndipo nikamwuliza anapoishi hakuna shule? Akasema ipo lakini hawalipi sasa akifundisha bure atakula nini?

Nikamuuliza, sasa ivi hufundishi unakula nini akakata simu! Mtu kama huyu ataendelea kulalamika kwamba ajira hakuna. Hajui kwamba kufanya kazi bure kunalipa zaidi kuliko kukaa bure kwa sababu ukifanya kazi bure, hizo 'connection' utazipata mwenyewe bila kutafutiwa.

Ninachokusudia kusema hapa ni kwamba Mwenyezi Mungu amemjalia kila mmoja wetu uwezo binafsi ambao mtu mwingine hawezi kuwa nao hata afanyeje lakini mara nyingi tunadharau kwa kufikiria na kutamani mambo makubwa ambayo hatuna uwezo nayo. Tazama Daudi alitumia jiwe kutoka mfukoni mwake kumpiga Mfilisti Goliati aliyekuwa na upanga na jeshi kubwa.

Je, fimbo au jiwe lako ni sanaa? Ni kuzungumza, kuandika, kuchekesha, kukimbia, kucheza mpira, kufuga au ni nini? Onyesha uwezo wako katika jambo unaloliweza nalo litakupa hizo 'connection' na litakupeleka ambapo hujawahi kutarajia kufika.

Jambo la tatu ni juu ya taarifa sahihi. Vijana wengi tumekuwa na utamaduni wa kufuatilia mambo mengi ya ovyo kuliko mambo ya msingi. Tunashinda mitandaoni tukiangaika kutazama vichekesho wakati hao wanaokuchekesha wameshagundua tayari mkononi wana nini na wanaingiza fedha kwa kufanya hivyo.

Lazima ufanye juhudi na wewe siku moja tukutazame na ukitaka itokee hivyo, lazima utafute taarifa muhimu na sahihi kutokana na kile unachokipenda.

Faida kubwa tuliyo nayo kwa sasa ni urahisi wa upatikanaji wa taarifa kuliko zamani lakini taabu yetu ni taarifa gani tunafuatilia. Dunia hii ya utandawazi taarifa zipo kama kokolo ni wewe uchague kama unataka sangara, sato, fulu, perege au kamongo, vyote vinapatikana.

Kwa mujibu wa Dk. Onesmo Matei (PhD) vijana wanatakiwa kufungua macho kuona fursa na kuchukua hatua.

Anasisitiza kuwa si kwamba fursa hazipo bali tatizo ni juu ya kuchukua hatua. Akaenda mbali zaidi akasema: "Si kuchukua hatua tu, lakini ni muhimu sana kujitofautisha yaani unafanya nini cha tofauti.

Haya aliyazungumza Machi 24, mwaka huu, tulipopata nafasi ya kutoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana katika chuo cha uongozi MSTCDC Arusha.

Mtaji, hiki kimekuwa kilio cha vijana wengi. Ni kweli lakini ukisoma kitabu cha Azimio la Arusha kuna mahali mwalimu Julius Nyerere ameeleza madhara ya kuona fedha ndiyo kila kitu na anasema fedha ni matokeo ya kazi, akimaanisha kuwa ili upate fedha inapaswa kutangulia kufanya kazi ndiyo maana hata mfanyakazi analipwa mwisho wa kazi kufanyika si mwanzo.

Akatolea mfano wa wabunge kwamba hata wawapo bungeni hawatoi njia mbadala za utatuzi wa changamoto za wananchi, badala yake kila mbunge akisimama anaidai serikali fedha za maendeleo.

Masuala ya kuwalaumu wazazi, ndugu na jamaa zako kwamba hawakukusaidia achana nayo yatakuchelewesha.

Kuwa na maono makubwa juu ya maisha yako ukitokea msaada utashukuru. Wako vijana wanalalamika hakuna ajira, ukimuuliza tangu umalize chuo umewahi kutembelea kiwanda kipi hata kuuliza tu kama kuna kazi yoyote, hakuna. Hatufanyi hivyo kwa sababu tuna uhakika wa kula nyumbani asubuhi, mchana na jioni na hatimaye kulala.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# "Kwenu ulikuwa huli hivyo, kula unenepe." Ni kauli ya mwanaume mwenye gubu



Na Adam Fungamwango

KWENYE maisha ya ndoa kuna mambo mengi mazuri na changamoto zake. Kijana yeyote anayechipukia, awe wa kiume au wa kike, akishafika wakati wa kubalehe anadhani kuwa siku akifunga ndoa basi itakuwa raha siku zote.

Ni kweli madhumuni ya ndoa siku zote ni hayo na kila mtu anatamani kuwa hivyo lakini wanaooana ni binadamu ambao hawajakamilika. Chochote kinaweza kutokea. Ndiyo maana wakati wa kufunga ndoa kila mmoja huulizwa kama anaweza kumvumilia mwenzake kwa shida na raha.

Shida inayosema hapo siyo kulala na njaa, au mume kukosa pesa ya kumtunza mke kwa sababu mbalimbali, lakini pia changamoto za kitabia kutoka kwa wote wawili.

Ndoa inafungwa na mtu anayetoka familia nyingine, yenye malezi na utamaduni wao, dhidi ya mwingine ambaye naye ametoka kwenye familia nyingine, mazingira mengine, maeneo mengine na tabia zingine. Hapo ndipo kuna changamoto.

Leo tutaangalia tabia mbaya za baadhi ya wanaume hasa waliooa. Ni kweli kila mtu ana tabia yake, lakini unapoishi na mtoto wa mtu unatakiwa kubadilika. Kuna msemo unasema tabia haina dawa. Ni kweli, lakini inabadilika kutokana na mazingira.

Na ndiyo maana mtu yeyote mwenye mpenzi mpya, kabla ya kufunga ndoa, hata akiwa na tabia mbaya vipi, kama anakunywa pombe kupita kiasi, au ana wivu kupita kiasi, mchoyo, atajitahidi sana kuficha ili zisionekane kwa mwenzake.

Zitaibuka tena pale watakapooana na kukaa pamoja. Kwa maana hiyo binadamu anaweza kubadilisha tabia yake kutokana na mazingira. Kwa nini mtu asibadilike?

Umemchukua mtoto wa watu kutoka kwenye mikono ya wazazi wake, unakuja kumnyanyasa, kumpiga, kumtukana na kumsimanga kama hana kwao. Mambo haya yapo kwenye jamii, ambapo wanawake wamekuwa hawana amani na hamu ya ndoa kutokana na mambo wanayofanyiwa na wanaume, hasa wanapoona kuwa wake zao wameshakuwa na watoto na hawawezi kuondoka.

Wanamuziki wameshaonya sana kuhusu tabia hiyo. Bendi ya Vijana Jazz ilitunga nyimbo mbili kwa nyakati tofauti juu ya wanaume wanaonyanyasa wake zao.

Tena bendi ya Vijana ilidili na wanaume ambao wanaongea sana, wasimangaji na kwa kiswahili kizuri wanaitwa wanaume wenye gubu.

Mtu mwenye gubu ni zaidi ya mwongeaji. Ni hali ya kukosoa kila kitu, kiwe kibaya au kizuri, asiyeridhika na chochote na hata, kama kila kitu kipo sawa atatafuta sababu ya kuongea tu. Wakati mwingine anataka kukuonyesha kuwa yeye ni zaidi na ndiye anakufanyia kila kitu, ili mradi tu ni tabia mbaya.

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, Vijana Jazz ilitunga kibao kiitwacho 'Gubu la Mume' ambacho kilitikisa sana kutokana na maudhui yake.

"Safiri salama kawasalimie wote na ukifika salama urudishe majibu mapema. Salamu sana kwa baba, salamu sana kwa mama, uwaeleze sijambo bali nimekonda kwa gubu la mume. Jambo dogo kwake kubwa, atasema kutwa nzima na usiku hatulali. Hakuna kitu ninachokosa huku nyumbani, kama chakula ninakula mpaka natupa, kama ni nguo ninavaa za kila aina, kutoka vitenge mpaka khanga hazinipiti, ila tu gubu la mume."

Ukisoma mashairi ya wimbo huu utagundua kuwa kweli ilikuwa zamani, kwa sababu hakukuwa na simu za mkononi, kwa hiyo mawasiliano ilikuwa ni mpaka mtu aende anakokwenda.

Mwanamke anamwambia dada yaka akawasalimie wazazi, lakini akifika huko arudishe majibu mapema. Kwa sasa ilikuwa ni suala la kutuma meseji tu. Anasema hakuna anachokosa nyumbani kwake, ila tatizo mume ana gubu sana.

"Japokuwa ana gubu nakuomba vumilia, shemeji yangu kweli ana gubu, hawezi kuiacha tabia hiyo. Hawezi kuiacha kabisa, kwa vile kazaliwa nayo, shemeji yangu kweli ana gumu, hawezi kuiacha tabia hiyo. Naomba naomba mvumilie, hasira weka pembeni, kila mume na tabia yake, na wengi wenzako hvumilia.

Wengine ni walevi sana, wengine hupiga sana na wengine wana wivu sana, lakini wenzako huvumilia."

Hapa ndipo utakapoona watu wa zamani na tungo zake zenye hekima na busara. Kwa sasa si mtunzi, au huyo ndugu angemwambia achane naye, mwanaume gani huyo, dai talaka yako. Lakini ndugu wa mwanamke huyo kwanza anachotaka ni kulinda ndoa, mpaka wazazi waingilie kati ndipo uamuzi upatikane, lakini kwa sasa avumilie.

Katikati ya miaka ya 1980, hao hao Vijana Jazz aliibuka na kibao kingine chenye maudhui yanayofanana na hayo, walichokiita 'Nilitaka Iwe Siri.' Kilitungwa na Cosmas Chidumule. Mtu na mkewe wameachana, lakini bwana anapita huku na huko kutangaza sababu za uongo za kwa nini waliachana. Mke alipoisikia, ndipo kwa uchungu akaweka mambo hadharani. Nilitaka iwe siri yetu, mimi nawe ee, sikutaka watu wafahamu nilichotutenganisha, wewe mtalaka wangu mzazi mwenzangu ee, ukaanza kunitangaza vibaya, mimi mama ooo.

Nimevumilia leo nitasema ieleweke, nani wa kulaumiwa kati yetu mimi nawe, ooo mama ooo.

Ninapokula ananisema mama oohooo, kwenu ulikuwa huli hivyo, kule unenepe mama. Akinunua nguo ananisimanga, kwenu ulikuwa hujui kuvaa, vaa upendeze dada, nikijipodoa anaicheka, mama oohoo, kwenu ulikuwa hupaki wanja, paka ujidai dada, Ninapokula unanisema mama oohooo."

Kwa hili alichokisema huyu mwanamama hapa kwenye wimbo huu, ni kwamba mwanaume huyu alikuwa na gubu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-6

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

TUNDA na Halima nao waliingia. Kipindi kaka yao Dan amefika walikuwa sokoni, ingawa alikuwa ameshawataarifu kwa simu kuwa atafika nyumbani.

Baada kumsalimia, walikwenda kuweka mifuko yao ya bidhaa walizokwenda kununua, wakarejea.

"We kaka we, kisa cha kutuletea ubaya wenzio kwa wifi yetu." Tunda alianza kama kawaida yake, huwa ana mdomo mwepesi zaidi kuliko dada yake Halima.

"We, acheni tu dada zangu, matatizo tu ya dunia."

"Ya dunia kaka, umetudhalilisha hapa mtaani kote. Miezi miwili iliyopita baadhi ya majirani zetu walitusindikiza kwenye ukumbi kwa ajili ya harusi. Leo bi harusi tu bado harusi haijajibu anakuja hapa kutulalamikia. Anasema una mwanamke mwingine ambaye sisi tunamjua..!

"Yaani kaka wifi kaja hapa kama kichaa, nywele, nguo alizovaa, hasira na sauti kali aliyokuwa nayo, kila mtu alikuwa anatuuliza yule uendawazimu umemuanza? Sisi tukasema wala, ni wifi yetu yule. Kama una mwanamke mwingine na amejua umeharibu." Halima alimkatisha mdogo wake na kuongeza kwa upole na masikitiko."

"Kwanza samahanini sana dada zangu. Kitendo cha nyinyi kuhusishwa kuwa mnamjua mwanamke wangu na ndiye mnamtambua kuwa wifi yenu na si Husna, ni kuwakosea heshima. Na hakikubaliki mbele hata ya Mwenyezi Mungu kwa sababu Husna ni mke wangu wa ndoa.

Lakini tatizo nimeshalijua kuna dada mmoja ndiye amefanya yote hayo, lakini nitakwenda kuyamaliza."

"Kaka twende wote tukamchambe maana atazoea siku nyingine, tutaenda kumsuta kwa rusha roho na mdundiko nyuma..."

"Hapana Tunda, yeye mwenyewe anatosha, kwa sababu alikuwa mpenzi wake kabla, wanaweza kukaa na kuelewana yakaisha. Ukienda tena na wewe kwenda kufanya ugomvi huko, yatazidi kuwa makubwa." Belo alimkatisha dada yake Tunda.

*******************************

"Wewe ulichokifanya unaona ni sawa? Unampigia simu mke wangu? Tayari umeshaniharibia ndoa yangu."

"Nimempigia simu saa ngapi na nimpigie ili iweje?

"Ulichokifanya Ziada siyo sahihi, umempigia simu mke wangu umemtupia maneno machafu, wewe unaona ndiyo sawa?"

"Mbona unaning'ang'aniza we baba vipi? Si uliniacha, ukaoa mwanamke mwingine, sasa mimi tena niko kimya na maisha yangu mengine umerudi tena kunitafuta la undani, kunitafuta ubaya."




**"Ya dunia kaka, umetudhalilisha hapa mtaani kote. Miezi miwili iliyopita baadhi ya majirani zetu walitusindikiza kwenye ukumbi kwa ajili ya harusi. Leo bi harusi tu bado harusi haijajibu anakuja hapa kutulalamikia. Anasema una mwanamke mwingine ambaye sisi tunamjua..!**

"Kwa hiyo nimekuacha sijakuoa wewe ndiyo ukaamua kumpigia simu mke wangu, si ndiyo?"

"Nimekwambia nimpigie simu ili iweje, mimi kama nakutaka si nakuwa mchepuko wako tu wakati uko kwenye ndoa, kwani ninashindwa?"

"Sasa yule ni kichaa aseme nimepigiwa simu?"

"Sasa kama kichaa au mwendawazimu mimi sijui."

Yalikuwa ni majibizano ya wapenzi wa zamani Dan na Ziada. Dan aliamua kwenda kabisa nyumbani kwa Ziada. Alikwenda bila taarifa. Hakutaka kumtaarifu kama atakwenda kwake kwa sababu alidhani kama amefanya jambo hilo hangeweza kumruhusu kwenda.

Hakutaka hata kumpigia simu kumtaka wakutane sehemu fulani kwa kuhofia kuwa Ziada asingekwenda kwani angehofia kutokana na kufanya tukio lile na kumpigia simu mkewe na kumpa maneno ya kejeli na dharau.

"Niambie ukweli Ziada kwa nini umefanya hivyo?" Akarudia tena akionekana haridhiki na majibu anayojibiwa.

"Nimekujibu na naendelea kukujibu kuwa sijawahi kufanya hivyo na sitofanya hivyo. Wewe si umeoa? Si una mke? Sasa mimi nianze tena kufuatilia mambo ya ndoa za watu?"

"Sasa mbona mke wangu kapigiwa simu na mwanamke, kamtukana, kamchamba, kamtisha kuwa hatokaa kwenye ndoa, sijui atamuonyesha...."

"Eee baba wewee, unajua Dan mimi nakuheshimu sana. Wewe ulikuwa mpenzi wangu, na hatukuwahi kugombana. Sasa usinilazimishe kwa sababu unakoelekea sasa siko. Kwa hiyo wewe ulivyosikia kuna mtu kamtukana mkeo basi ni mimi tu?

Ina maana hakuna mtu mwingine? Mimi ndiyo nina matusi sana au ndiyo nimekasirika sana, au nina wivu sana wewe kuoa, au vipi?" Akajibu Ziada akizidi kupandisha hasira.

"Mimi sina nia mbaya Ziada, nataka tu nijue nani amefanya hivi na nisawazishe mambo tu yaishe, hebu angalia ndoa yangu bado changa sana. Hivi ivunjike si aibu hii. Mke wangu tayari kesharudi kwao na anataka talaka."

"Dan, bado hujajibu swali langu, mimi ndiyo umeona mtu wa kumpigia simu mkeo na kumtukana, au amekwambia kuwa aliyemtukana anaitwa Ziada?"

"Hapana."

"Au kakwambia sauti yake inafanana hivi na wewe ukaona hii ni ya Ziada?"

"Hapana."

"Kumbe?"

"Samahani lakini kwa hili nitakaloongea. Unajua wewe mwanzo ulionekana hutaki mimi nioe na ulinilazimisha sana nikuoe na ulionekana kuchukia sana mimi kufunga ndoa mpaka hukuja kwenye harusi, nikajua una kinyongo, ndiyo maana lilipokuja hilo akili ikanijia kuwa ni wewe..." Dan akakatishwa na kicheko dhaifu cha kejeli kutoka kwa Ziada.

"Yalikuwa zamani baba, kwa sasa na mimi nina mchumba, anatarajia kunioa mwezi wa saba, tena bora umekuja nikupe na kadi kabisa unichangie mpenzi wangu wa zamani." Ziada akionekana kupunguza sauti kali ya mwanzo, sasa aliongea maneno kama mzaha hivi, lakini yalionekana kuwa ni kweli anamaanisha. Halafu akaendelea.

"Halafu unasikia, hapa tunavyoongea tumalize tu, mchumba wangu anaweza kufika hapa yakawa makubwa."

Dan hakutaka kabisa kuamini kuwa Ziada hakufanya kitu kama hicho. Kichwani akawa anajiuliza kama siyo yeye huyo aliyefanya kitu hiki ni nani? ukimuondoa Ziada hakuna hawara yake hata mmoja anayemhisi.

Akili ikaendelea kumtuma kuwa aliyefanya hivyo ni yeye Ziada, ila kwa sasa anavunga hasa baada ya kuona tayari ameshavuruga ndoa sasa ipo harijojo.


"Haya mama mimi naondoka, lakini naendelea kufanya uchunguzi wangu, kama wewe utakuwa unahusika, basi lazima nilipe kisasi. Na mimi nitavuruga huo uchumba wako na huyo mpenzi wako." Dan alinyanyuka baada ya kumaliza kuongea maneno hayo na kuanza kupiga hatua kutoka nje.

"Nakwambia hivi, rudi kambembeleze mkeo arudi nyumbani, wewe ni mwanaume. Mwenzangu miezi miwili tu umeanza kuchoka ee, na bado.

Hayo ndiyo maisha ya ndoa, hayana raha peke yake, yana raha na karaha. Dan ngome ya fitina haivunjwi na watu fitina.

Hivi hukumwambia kuwa mtakapooana mtafanya sherehe, lakini maisha ya ndoa ni magumu uvumilivu unahitajika?" Dan alisindikizwa na maneno hayo kutoka kwa Ziada. Yalikuwa ni maneno ya hekima, lakini ndani yake ni kama mzungumzaji aliyazungumza kwa namna ya dhihaka na mzaha.

**ITAENDELEA JUMAPILI**





# Kifua cha Willy Paul gumzo

MSANII wa muziki wa kizazi kipya kutoka Kenya, Willy Paul, ametangaza nia yake ya kuacha muziki na kujitosa katika masumbwi.

Mwanamuziki huyo ambaye katika siku za hivi karibuni amekuwa akitisha mitandaoni kwa kupakia picha na video zikimuonesha akichukua mazoezi ya kutanua misuli kwa kunyanyua vyuma, amesema kwa kuanzia atajiunga katika mchezo wa mieleka.

Hivi karibuni Paul ameibua gumzo baada ya picha zake kujadiliwa na mashabiki zake kutokana na jinsi alivyoumuka kifua.





# DR KAREEM APAKUA 2 MPYA

**Na Halfani Chusi**

MSANII anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Dr Kareem, ameachia ngoma mbili kali ambazo zimeanza kuwa gumzo.

Ngoma hizo mbili ameaziachia siku nne zilizopita ambazo ni Nichumu ambayo ni Video na Acha ambayo imewekwa katika mfumo wa Audio.

"Ninawaomba wadau wa mziki na mashabiki zangu kuniunga mkono kazi zangu zinapatikana kwenye platform zote Youtube kwa jina la Dr Kareem, pia Spotify, Apple music na Audimarck" amesema

## ZISIKUPITE

### GAVI KUIKAMUA CHELSEA

KLABU ya Chelsea iko tayari kumfanya kiungo wa kati wa Barcelona na Hispania, Gavi kuwa miongoni mwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi kwenye Ligi Kuu England ili kumsajili kinda huyo mwenye umri wa miaka 18. (***AS***)

### OSIMHEN ANUKIA CHELSEA

CHELSEA pia ina imani inaweza kushinda mbio za kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24. (***90min***)

### ALLISTER ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imemfanya mchezaji wa kimataifa wa Argentina na Brighton, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 24 kuwa mlengwa mkuu kama kiungo wa kati kuelekea msimu mpya. (***Football Insider***)

### ZAHA AWAKATAA WAARABU

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 30 anatazamiwa kukataa kuhamia Saudi Arabia na kusalia Ulaya mara tu atakapokuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. (***Evening Standard***)

### KANE AISUBIRI SPURS

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 atasubiri kutathmini mkataba mpya wa Tottenham Hotspur mara tu klabu hiyo itakapomteua kocha mpya, huku Manchester United na Bayern Munich zikiwa na nia ya kumsajili. (***90min***)

### CITY, LIVERPOOL VITANI

KLABU za Manchester City na Liverpool zinawania kumsajili mlinzi wa Chelsea, mwenye umri wa miaka 20, Levi Colwill, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Brighton. (***Standard***)

### GALLAGER ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL pia inavutiwa na viungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23 na Mason Mount mwenye miaka 24. (***Football Insider***)

### AMORIM ANUKIA CHELSEA

CHELSEA imefanya mazungumzo na Ruben Amorim wa Sporting Lisbon mwenye umri wamiaa 38, huku msako wa klabu hiyo wa kutafuta kocha mpya wa kudumu ukiendelea. (***Guardian***)

### GUNDOGAN KUTUA BARCA

BARCELONA inakaribia kufikia makubaliano na nahodha wa Manchester City na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32. (***90min***)

### MOTTOH AINGIA SOKONI

MANCHESTER City ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia winga chipukizi wa Portsmouth, Koby Mottoh, mwenye umri wa miaka 16. (***Football Insider***)

### CHELSEA KUMUUZA PULISIC

CHELSEA inaweza kuuza wachezaji wake tisa wa kikosi cha kwanza akiwamo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Marekani, Christian Pulisic, mwenye umri wa miaka 24. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GAVI AZIGONGANISHA CHELSEA NA BAYERN

## ●●● Hali mbaya ya kifedha ya Barca inatajwa inaweza kuchangia kuondoka kwa...

**LONDON,** England

CHELSEA na Bayern Munich zimeripotiwa kuwasiliana na kiungo wa kati wa Hispania, Gavi huku kukiwa na wasiwasi hali ya kifedha ya Barcelona itamaanisha hawawezi kumbakisha.

Gavi mwenye umri wa miaka 18 ni mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kuwa viungo wa kati bora zaidi duniani, akiwa tayari amecheza mechi 87 za wakubwa akiwa na Barcelona tangu aanze kucheza msimu wa 2021-22.

Kwa mujibu wa AS, nyongeza ya mkataba aliyosaini Gavi msimu huu ili kumfunga Barcelona hadi mwaka 2026 ilikataliwa na LaLiga kwa sababu ya hali ya kifedha za klabu hiyo na iwapo watashindwa kuweka nafasi ya kutosha ya mshahara ifikapo Juni 30, mwaka huu, Gavi ataruhusiwa kuondoka kwa uhamisho wa bure.

AS imeripoti Chelsea tayari imekutana na wakala wa Gavi katika kujaribu kumshawishi kuhusu uhamisho wa kwenda Ligi Kuu England, na mkutano wa pili unatarajiwa huku mmiliki wa Chelsea, Todd Boehly na wazazi wa Gavi wakihudhuria.

Ripoti hiyo inaeleza Chelsea iko tayari kumfanya kijana huyo mwenye mechi 19 za Ligi Kuu Hispania kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika Ligi Kuu England - zaidi ya mkataba aliosaini na Barcelona.

Wakati huo huo, Sport imeongeza Bayern Munich pia imemtahadharisha wakala wa Gavi wako tayari kuwasilisha ofa muhimu ikiwa ataruhusiwa kuondoka bila malipo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 553,

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 2.30
X | 3.10
2 | 2.35

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUNDOGAN AKANUSHA KUHAMIA BARCA



**MANCHESTER,** England

WAKALA wa Ilkay Gundogan amekanusha ripoti kuwa nahodha huyo wa Manchester City amekubali kujiunga na Barcelona.

Gundogan amebakiza zaidi ya miezi miwili katika mkataba wake na City, na imeripotiwa anakaribia kujiunga na Barca kama mchezaji huru kwa mkataba wa miaka miwili na chaguo la miezi 12 zaidi.

Hata hivyo, Ilhan Gundogan, mjomba na wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amepuuza mapendekezo ya kiungo huyo wa Ujerumani tayari ameamua kujiunga na viongozi hao wa LaLiga.

Aliiambia AS: "Nimeshangaa habari kuhusu makubaliano kufungwa wiki nyingi zilizopita.

"Bado hakuna makubaliano na klabu yoyote. Bado haijaamuliwa atacheza wapi katika miaka ijayo."

Aliongeza: "Ilkay bado anaweza kushinda mataji matatu makubwa msimu huu akiwa nahodha wa Manchester City. Hilo ndilo jambo pekee analozingatia kwa sasa."

Gundogan ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu England tangu ajiunge na City akitokea Borussia Dortmund mwaka wa 2016, pia amebeba Kombe la EFL mara nne na Kombe la FA mwaka 2019.



## *Martinez nje msimu wote*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imethibitisha kuwa Lisandro Martinez hatakuwepo katika kipindi kilichosalia cha msimu huu baada ya kuumia wakati wa sare ya Alhamisi ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla.

Martinez alibebwa kutoka uwanjani na Marcos Acuna wa Sevilla na Gonzalo Montiel, wachezaji wenzake wa Argentina - baada ya kuumia katika mechi za mwisho Old Trafford.

Huku Erik ten Hag akiwa tayari ametumia wachezaji wake wote wa akiba, United walilazimika kumaliza mchuano wa mkondo wa kwanza wa robo fainali wakiwa na wachezaji 10 na Sevilla walichukua fursa ya kupata sare ya 2-2.

Mashetani Wekundu hao Ijumaa walithibitisha beki wa kati, Martinez hatacheza tena katika msimu huu 2022-23.

"Lisandro Martinez ameondolewa kwa muda uliosalia wa msimu baada ya kuvunjika mfupa wa mguu wake," taarifa ya klabu ilisema.

"Hata hivyo, beki huyo wa Argentina anatarajiwa kupata ahueni kamili kwa wakati ili kuwa tayari kwa ajili ya kuanza kwa msimu ujao."

# HABARI MICHEZO


549,430

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/04/23 | 17:00 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 2.73 | 3.31 | 2.40 |
| 02. 19/04/23 | 17:00 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 03. 19/04/23 | 18:00 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 04. 19/04/23 | 20:30 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 05. 19/04/23 | 21:45 | Blackburn vs Coventry | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 19/04/23 | 21:45 | Swansea vs Preston | 2.44 | 3.16 | 2.76 |
| 07. 19/04/23 | 22:00 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.41 | 2.48 |
| 08. 20/04/23 | 20:30 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 09. 20/04/23 | 22:00 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 10. 21/04/23 | 01:00 | San Lorenzo vs Fortaleza CE | 2.21 | 3.17 | 3.43 |
| 11. 21/04/23 | 05:00 | Universitario vs Goias | 2.23 | 3.12 | 3.01 |
| 12. 21/04/23 | 05:00 | Deportes Tolima vs CA Tigre | 2.27 | 3.28 | 3.17 |
| 13. 21/04/23 | 19:00 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.44 | 3.27 | 2.74 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 16/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5406 | Lecce vs Sampdoria | 1.91 | 3.15 | 4.00 |
| 14:00 | 3477 | Lille vs Montpellier | 1.49 | 4.30 | 5.39 |
| 14:00 | 3726 | Shakhtar Donetsk vs FK Lviv | 1.14 | 6.36 | 13.34 |
| 15:00 | 4416 | Girona vs Elche | 1.48 | 4.11 | 5.81 |
| 16:00 | 2057 | West Ham vs Arsenal | 5.39 | 4.00 | 1.53 |
| 16:00 | 2434 | Clermont Foot vs Angers | 1.78 | 3.60 | 4.00 |
| 16:00 | 2761 | AIK Football vs Hammarby | 2.78 | 3.19 | 2.29 |
| 16:00 | 3023 | AJ Auxerre vs Nantes | 2.38 | 3.01 | 2.96 |
| 16:00 | 3149 | Torino vs Salernitana | 1.71 | 3.35 | 4.81 |
| 16:00 | 3330 | Brest vs Nice | 3.00 | 3.15 | 2.27 |
| 16:00 | 5194 | Strasbourg vs AC Ajaccio | 1.74 | 3.26 | 4.82 |
| 16:00 | 5738 | Astana vs Kairat Almaty | 1.37 | 4.10 | 6.00 |
| 16:30 | 5461 | Werder Bremen vs SC Freiburg | 2.61 | 3.31 | 2.48 |
| 17:00 | 1949 | Mechelen vs KAA Gent | 4.61 | 3.86 | 1.64 |
| 17:00 | 2142 | Copenhagen vs Viborg FF | 1.47 | 4.34 | 6.05 |
| 17:00 | 3694 | Simba vs Young Africans | 2.30 | 3.10 | 2.35 |
| 17:00 | 4103 | Bohemians vs Mlada Boleslav | 2.37 | 3.39 | 2.75 |
| 17:00 | 4558 | Dundalk FC vs Derry City | 3.69 | 3.33 | 1.86 |
| 17:15 | 4476 | Getafe vs Barcelona | 5.30 | 3.51 | 1.62 |
| 17:30 | 2304 | FC Basel vs BSC Young Boys | 3.21 | 3.42 | 2.08 |
| 17:30 | 5454 | Grasshoppers vs FC Sion | 1.93 | 3.53 | 3.53 |
| 17:45 | 1740 | Cambuur vs Feyenoord | 8.59 | 5.39 | 1.27 |
| 18:00 | 1343 | Odd Ballklubb vs Brann | 3.99 | 3.68 | 1.78 |
| 18:00 | 2686 | Bodo Glimt vs Stabaek | 1.24 | 5.88 | 9.24 |
| 18:00 | 3943 | Molde vs Rosenborg | 1.57 | 4.04 | 4.93 |
| 18:05 | 4301 | Monaco vs Lorient | 1.37 | 4.90 | 6.40 |
| 18:30 | 2266 | Union Berlin vs VfL Bochum | 1.57 | 3.75 | 5.39 |
| 18:30 | 4538 | Nottingham vs Manchester Utd | 4.51 | 3.60 | 1.69 |
| 18:30 | 4988 | Olimpija Ljubljana vs Maribor | 2.19 | 3.28 | 2.87 |
| 19:00 | 1999 | Ujpest FC vs Paksi FC | 2.26 | 3.48 | 2.70 |
| 19:00 | 3186 | Sassuolo vs Juventus | 3.44 | 3.20 | 2.05 |
| 19:00 | 3966 | Rostov vs Zenit St Petersburg | 4.70 | 3.92 | 1.61 |
| 19:00 | 5657 | HNK Rijeka vs Hajduk Split | 2.48 | 3.24 | 2.51 |
| 19:30 | 1825 | Royal Antwerp vs Kortrijk | 1.27 | 5.25 | 9.28 |
| 19:30 | 5395 | Atletico Madrid vs Almeria | 1.22 | 5.60 | 10.99 |
| 20:00 | 4688 | Sporting Braga vs Gil Vicente | 1.35 | 4.92 | 7.23 |
| 20:15 | 3332 | Union Saint Gilloise vs RFC Seraing | 1.11 | 8.26 | 16.13 |
| 20:15 | 3934 | Valerenga vs Sarpsborg | 2.05 | 3.42 | 3.27 |
| 20:30 | 4071 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.35 | 2.37 |
| 20:30 | 5717 | Trabzonspor vs Besiktas | 2.79 | 3.31 | 2.36 |
| 21:00 | 3497 | Fortuna Sittard vs AZ Alkmaar | 4.40 | 3.60 | 1.71 |
| 21:00 | 4983 | Ajax vs Emmen | 1.11 | 8.20 | 14.99 |
| 21:45 | 3162 | Marseille vs Troyes | 1.19 | 6.21 | 11.03 |
| 21:45 | 4874 | Roma vs Udinese | 1.83 | 3.29 | 4.19 |
| 22:00 | 1702 | Corinthians vs Cruzeiro | 1.63 | 3.49 | 4.98 |
| 22:00 | 2120 | Valencia vs Sevilla FC | 2.12 | 3.16 | 3.31 |
| 22:00 | 2594 | Flamengo vs Coritiba | 1.35 | 4.47 | 7.35 |
| 22:15 | 5537 | Valur vs Breidablik | 3.22 | 3.64 | 1.94 |
| 22:30 | 2415 | Sporting Lisbon vs FC Arouca | 1.18 | 6.41 | 12.02 |
| 23:30 | 2706 | LA Galaxy vs Los Angeles FC | 2.82 | 3.40 | 2.37 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM FC YAZINDUKA LALA SALAMA LIGI KUU

**Na Hadija Mngwai**

ZIKIWA zimebakia mechi nne ili kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/2023, uongozi wa Azam FC umesema kila mechi kwao sasa ni sawa na fainali na wanataka kuzibeba pointi zote 12.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Azam FC iko katika nafasi ya nne ikiwa na pointi 50 huku wapinzani wao Singida Big Stars wakiwa nafasi ya tatu na pointi 51 kibindoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabiti Zakaria 'Zaka za Kazi' alisema wanajipanga kuhakikisha wanashinda michezo yote iliyobakia na kampeni hiyo wataianza watakapoikabili Ruvu Shooting.

"Kwa sasa tunaangalia mechi moja moja kwa kufanya maandalizi makini, ikiisha mechi ya kwanza tunaangalia mechi inayofuata, kila mchezo kwetu ni muhimu, tunauchukulia kama fainali. Hali ilivyo hatuwezi kujihakikishia nafasi ya tatu au nne, " alisema Zaka.

Alisema wanataka kuona wanashinda mechi hizo huku wakiiombea Singida Big Stars kupoteza angalau pointi moja ili wao wamalize kwenye nafasi ya tatu.

"Singida wakishinda mechi zao zote na sisi tukashinda zote hatuwezi kuwapata, hivyo kwa sasa tunajiandaa na mchezo wetu dhidi ya Ruvu Shooting tutakaocheza Aprili 22, na tukimaliza huo tunajiandaa na mchezo unaofuata, hatutaki kujichanganya," alisema ofisa huyo.

Aliongeza kikosi chao kipo vizuri, wachezaji wote wameendelea na mazoezi na wanaamini mambo yatakwenda sawa sawa.



Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro (kushoto), akizungumza kuhusu usalama kuelekea mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 11:00 jioni. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# *Ni siku ya hukumu*

INATOKA UK 24

si kwa Afrika Mashariki tu, bali ni Afrika nzima, hivyo hawatakuwa tayari kupoteza mbele ya mashabiki zaidi ya 50,000.

Kaze alisema wanaingia uwanjani bila presha na anaamini wapinzani wao ndio wana wasiwasi kwa sababu wakipoteza watawapa nafasi kubwa ya kutangaza ubingwa.

Kuhusu kiwango cha mshambuliaji wao tegemeo, Fiston Mayele, alisema ubora wa nyota huyo ni mkubwa na si uwanjani tu, hata anapokuwa na wenzake anawahamasisha wawe na hali ya kujiamini ili kufanya vizuri.

"Kikosi cha Simba kipo vizuri katika safu ya ushambuliaji lakini kwa kuwa tunacheza kama timu, ninaimani tunaweza kuwazuia kutopata nafasi ya kufunga," alisema Kaze.

Aliahidi kikosi chake kimejipanga kutoa burudani stahiki kwa mashabiki na wanachama wao kwa kiwango kizuri ili kupata matokeo bora yatakayowapeleka kwenye malengo.

"Tumejiandaa kucheza kama timu yaani tutalinda kama timu mpaka kushambulia kama timu kwa utulivu na umakini mkubwa sana ili kupata pointi tatu muhimu katika hii dabi," Kaze alisema.

Mudathir Yahya, kiungo wa Yanga, alisema wapo tayari kwa mapambano na wamejiandaa kufanya vizuri katika mechi hiyo.

"Hatuna presha, tunautaka ubingwa na tukishinda katika mchezo huo tunakuwa mabingwa, tupo vizuri na tutaendelea kuwa bora na tunaamini itakuwa dabi ngumu kwa kuwa ndio tutatakiwa kutangaza ubingwa mbele ya mpinzani," alisema Mzanzibari huyo.

# Mayele, Chama gumzo

INATOKA UK 24

Deus Kaseke wa Singida Big Stars, Shomari Kapombe, Mzamiru Yassin na Mohames Hussein 'Tshabalala' wote wa Simba na Shiza Kichuya wa Namungo wote hao wakiwa na 'assist' tano kila mmoja.

Katika eneo la 'clean sheets', baada ya Diarra golikipa anayefuatia ni Aishi Manula wa Simba (12), Ally Ahmada wa Azam FC (8), Metacha Mnata wa Yanga (7), Mahmoud Mroivil wa Coastal Union, Fikirini Bakari wa Ihefu na Said Kipao wa Kagera Sugar kila mmoja ana 'clean sheets' tano.

Michezo
Nipashe
Jumapili Aprili 16, 2023



Gavi azigonganisha Chelsea na Bayern UK. 21




Mayele

Baleke

# NI SIKU YA HUKUMU

Na Saada Akida

## ●●● Yanga yahitaji pointi tano, Simba yaahidi kuvuruga hesabu katika...

WANASEMAJE, ni kauli inayosubiriwa kutoka kwa mashabiki wa soka nchini baada ya kumalizika mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga inayotarajiwa kuchezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba itawakaribisha Yanga ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 waliyopata katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Oktoba 23, mwaka jana.**

Mnyama anahitaji kuvunja mwiko wa kutopata ushindi katika mechi saba mfululizo huku Yanga wakitaka kuendelea kusaka pointi tatu wakiwa wamecheza michezo 22 bila ya kupoteza na kujihakikisha ubingwa wa msimu huu.

Timu hizo zinakutana zikiwa na utofauti wa alama nane, Yanga ambao ni mabingwa watetezi wakiwa kileleni na pointi 68 kibindoni huku Simba yenye pointi 60 ikifuatia.

Kuelekea mechi hiyo ya dabi, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema anajivunia ubora wa safu yake ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikifanya vizuri chini ya uongozi wa Jean Baleke, ambaye leo atakuwa anacheza mchezo wa kwanza dhidi ya watani zao.

Robertinho alisema maadalizi ya mchezo huo yapo vizuri na anaamini watafanya vizuri katika mechi hiyo ili kuhakikisha wanajiweka sehemu salama kuelekea kwenye mbio za ubingwa.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kufanya vizuri na wanatambua endapo watafungwa katika mchezo huo, tayari watawapa ubingwa wapinzani wao jambo ambalo hawapo tayari kuona linatokea.

"Simba hatutaenda kubadili aina yetu ya uchezaji kwa sababu mechi ya Yanga ni kama mechi nyingine tu, wachezaji wana morali na wanautaka mchezo. Malengo yetu ni kucheza vizuri na kushinda. Tuna Baleke (Jean), sasa tunajivunia sana, Mohammed Hussein, Shomari (Kapombe) wana uwezo mkubwa, nimezungumza na wachezaji wameniahidi kufanya vyema kesho (leo) , tunawaheshimu Yanga," alisema Robertinho.

Aliongeza lengo la Simba ni kubeba pointi tatu za mechi hiyo huku wakiingia uwanjani wakifahamu vizuri wapinzani wao na amewalekeza nyota wake kucheza soka litakalowafurahisha mashabiki wao.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Hussein, alisema benchi la ufundi limemaliza kazi yake na wao kama wachezaji wamepokea walichofundishwa mazoezini na sasa wanakwenda kukamilisha mchezo.

"Tunatambua tukifungwa tunawapa ubingwa wenzetu na sisi hatupo tayari kuwapa ubingwa kwa kuwa tunautamani, tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi," alisema beki huyo.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema mechi hiyo ni kubwa na

INAENDELEA UK 23

# Mayele, Chama gumzo

Na Adam Fungamwango

WAKATI timu zao zikitarajiwa kukutana katika mechi ya dabi leo, wachezaji wa Clatous Chama, Fiston Mayele, Saido Ntibazonkiza na Djigui Diarra wameendelea kutamba katika Ligi Kuu Tanzania Bara kila mmoja akishikilia rekodi yake.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Mayele, straika wa Yanga anaendelea kuongoza katika orodha ya wafungaji akiwaacha wenzake kwa mbali baada ya Jumanne iliyopita kufikisha mabao 16.

Kwenye eneo la kutoa pasi za mwisho za mabao 'assist', Chama wa Simba bado ni mfalme akiwa ametoa pasi 14 zilizozaa mabao, akiwaacha wengine maili nyingi.

Kipa wa Yanga, Diarra ni kinara wa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean sheets' Jumanne iliyopita dhidi ya Kagera Sugar akitimiza mechi 15, huku kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, akiwa ndiye mchezaji aliyechangia mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, yaani ya kufunga yeye mwenyewe na yale aliyotoa pasi za mwisho.

Ntibanzokiza, raia wa Burundi amepachika mabao 10 mpaka sasa, sita akiyafunga akiwa Geita Gold na manne akiwa Simba, akiwa pia na 'assist' tisa, hivyo kuwa na mchango wa mabao 19.

Wakati Mkongomani Mayele ana mabao 16, Saido na Moses Phiri wote wa Simba wana mabao 10 kila mmoja, Bruno Gomes wa Singida Big Stars, John Bocco wa Simba na Sixtus Sabilo wa Mbeya City, wote kila mmoja akifunga mabao tisa.

Wakati Mzambia Chama anatamba na 'assist' zake, anafuatiwa na Saido mwenye tisa, Ayoub Lyanga wa Azam akiwa nazo saba, Sabilo wa Mbeya City na Nicolaus Gyan wa Singida Big Stars wakiwa 'assist' sita kila mmoja huku Ally Ramadhani 'Kagawa' wa Kagera Sugar,

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >